OKTOBA MMXXV - TOLEO LA XLVII

# NGURUMO
## ya Mwandishi




**HABARI KUU:**

- Tuzo ya Nobel ya Fasihi 2025

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
TUILINDE TANZANIA

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
BASHIRU ABDALLAH

**NEW IN TOWN: Uk 04**
KOSA LA SIRI na JAMHURI YA PLATO

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
CHUNGU TAMU—2

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UPATAZO

**MAKALA: Uk 08 - 09**
KITABU HIKI WAPASWA KUWA NACHO

**KUTOKA KWA FANANI: Uk 10**
KAMBA ZA FRANK MASAI

**SAKO KWA BAKO – Uk 11**
KHADIJA ABDUL

**RIWAYA: Uk 12—13**
MSALITI '9'

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '9'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
Alibaba na Wezi 40 '24'

**HABARI MOTO: Uk 17**
TUZO YA NOBEL YA FASIHI 2025

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
KITABU CHA 'THE DIVINE COMEDY'

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
MENO YA MBWA

**MATANGAZO: Uk 22**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**
NCHI YANGU TANZANIA / GEN Z

**HABARI PICHA: Uk 20**

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**

**ELIMU JAMII: Uk 24 & 25**
SAFARI YA MALEZI (5): TECHNOLOJIA NA MALEZI

**HADITHI: Uk 26 - 27**
Happy New Year '11'

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '06'

## TAHARIRI:
# Tuilinde Tanzania

Amani iwe kwenu!

Nakuandikieni ndugu zangu Watanzania, hususan vijana, kwa heshima na taadhima. Ni mara nyingine tunakutana jaridani kama ilivyo ada. Lakini safari hii kwa uchungu na huzuni juu ya Mama yetu Tanzania.

Kwanza nikupongezeni kwa kupiga kura ya kumchagua Rais, wabunge na madiwani wa kuliongoza taifa letu. Hii imeonesha ukomavu wenu wa kisiasa. Kwa hili, tujipongeze!

Ndugu zangu Watanzania, sintofahamu iliyojitokeza wakati wa uchaguzi hakika imelitia doa taifa letu, na imeitia doa amani yetu tunayojivunia mbele ya uso wa kimataifa. Sote tunajua kuwa tunahitaji mabadiliko, ndiyo. Lakini si kwa njia hiyo tuliyoamua kuitumia. Haikufaa na haifai hata kidogo!

Ukirejelea historia ya taifa letu, Tanganyika tulipata uhuru wetu kikatiba, hivyo basi, kama tulivyoanza twapaswa kuendelea jinsi ileile. Hata mabadiliko tunayohitaji twapaswa kuyadai na tutayapata kwa mazungumzo na si vurugu. Kuandamana si kuvunja maduka, kuandamana si skuiba mali za wengine.

Amka Tanzania! Si kila mtu anapenda utulivu tulio nao, tahadhari ni muhimu sana kwetu na kwa vizazi vinavyotufuata, kama tulivyoachiwa na baba zetu, basi nasi ni jukumu letu kuwarithisha watoto wetu taifa lenye amani.

Kuipoteza amani ni jambo jepesi sana, lakini kuirudisha yaweza kuchukua miaka na mikaka. Tutapoteza ndugu na jamaa, tutaacha watoto yatima. Historia itataja tarehe ya pale tulipoanza kuichokonoa amani yetu lakini haitaweza kutabiri ni lini itarudi.

Maandamano ya amani na mazungumzo ni njia sahihi ya kupata kila tunachohitaji. Amini katika mazungumzo siku zote. Chonde chonde vijana, tusikubali kutolewa sadaka juu ya madhabahu ya mwendawazimu!

Tutunze amani yetu, tuilinde Tanzania!

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## MWANDISHI WETU:
## BASHIRU ABDALLAH

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

**Leo katika safu yetu ya Mwanishi Wetu, tunamleta kwenu mwana-ushairi kutoka Zanzibar-Dar. Kijana huyu mshititi katika uga wa ushairi ni mshindi wa diwani bora ya Kiswahili katika Tuzo ya Pan Africa Writers Association (PAWA) kwa kitabu chake cha Wino wa Dhahabu.**



B.A: Naitwa Bashiru Abdallah, mzaliwa wa Ujiji mnamo Mei 8, 1992. Ni mtoto wa kwanza katika familia ya watoto saba. Ninaishi na familia yangu jijini Dar es salaam lakini muda mwingi napatikana visiwani Zanzibar.

Nikiwa nasomea masomo yangu ya uhasibu, kupitia Facebook, nilibahatika kukutana na shairi ambalo nililipenda sana . Ninachokikumbuka bila wasiwasi, ni shairi la “Niombaye” la Alhaj Osan Omari Ngulangwa ambalo nililinakili na kuliwekea gamba gumu kwa kulipenda na kuvutwa na ujumbe wake na mtiririko wa mada iliyowasilishwa.

Shairi langu la awali nililiandika mnamo Februari 23, 2015 ambapo ilikuwa miezi michache baada ya kuhitimu na miezi michache kabla ya kufunga ndoa. Shairi lile lenye anuani ya “Umbali Sio Sababu” ni kielelezo na jawabu la swali la “Kwanini nilianza kuandika mashairi? Na Kwanini iwe mashairi ya Kiswahili?”
Ni kupitia ushairi wa Kiswahili ndipo niliona wepesi na jambo aali na muruwa la kuwasilisha hisia zangu kwa niliyetaka zimuingie.


Pongezi kwa ndugu yangu Ahmadi Kabezi ambaye ndiye aliyenihimiza kuandika kwa ajili ya ulimwengu ambao uko nje yangu na ahli yangu. Na hapo ndipo nilianza kuandika mashairi mengi yenye maudhui mbalimbali hadi kufikia hatua ya kushiriki baadhi ya mashindano makubwa na kushika nafasi za juu kwa nyakati tafautitafauti.

Hadi kufikia sasa nimeshachapisha diwani 5 peke yangu na 1 ambayo nimeshirikiana na watunzi wengine 33. Baadhi ya diwani zangu zinapatikana jijini Dar es salaam TPH Bookshop - Mkuki na Nyota (Posta) na visiwani Zanzibar Alif Publications (Mkunazini). Lakini pia diwani zote nasambaza mwenyewe kwa wahitaji au wasomaji ambao watawasiliana nami moja kwa moja au kupitia familia ya wasomaji na waandishi wa vitabu.

Uandishi wa mashairi ni fani adhimu, nii kipawa ambacho kama ukijaaliwa kugundua au kuambiwa unacho, basi unahitaji kazi ya ziada kukilea na kukikuza kipawa hicho. Na njia kuu ya kukilea na kukikuza kipawa cha uandishi wowote ule ni kusoma sana kazi za utanzu husika au tanzu nyingine ambazo zinashabihiana. Kwani kupitia njia hiyo ndipo utaweza kuwa tajiri wa lugha, fikra, na hata kujua namna gani nawe kama mwandishi unaweza kuja na namna, mitindo na miundo mipya mizuri ya kibunifu ambayo itakurahisishia kufikia ujumbe unaoukusudia.

Ngurumo ya mwandii tunakushukuru sana kwa neno lako. Tunakuombea heri katika yote ufanyayo.

## NEW IN TOWN :
## KOSA LA SIRI na JAMHURI YA PLATO





**Mwandishi: Ben Mkota**

"… kuna *new twist* ama sijui niite *new development* katika kesi yako. Amejitokeza mama fulani na kukiri kwamba ndiye aliyehusika na kwamba alikusingizia tu kosa lile… kwa hivyo, waziri ametoa agizo uachiliwe huru *with immediate effect!*"

Auni anaupata tena uhuru wake baada ya kutumikia kifungo jela kwa takribani miaka thelathini kwa kosa ambalo inavyokuja kubainika, hakulifanya. Badala ya kuufurahia uhuru ule, moyo wake unaumia zaidi kwa ufichuzi kwamba kuhukumiwa na kufungwa kwake kulikuwa kosa, na kulimfanya apoteze kila alichokithamini maishani. Sababu inayotolewa ya kumweka huru vilevile inamwacha na maswali mengi kuliko majibu.

Je ni nani huyo aliyemsingizia kosa lile? Kwanini alimsingizia kosa hilo? Kumsingizia kosa hilo kulilenga kuficha siri gani?

Jikamatie nakala yako sasa kwa Tsh 10,000 tu.
Piga simu namba




Kwa mara ya kwanza katika historia, utasoma JAMHURI YA PLATO, Tafsiri ya Mwalimu Julius Nyerere.

Hii ni kazi yake ya mwisho kuandika kabla ya kuiaga dunia. Haikuwahi kuchapishwa, haikujulikana nje ya duru za wasomi mpaka sasa!

Ni zaidi ya kitabu; ni dirisha la kuangalia namna Baba wa Taifa alivyoendeleza mjadala wa haki, uongozi na jamii bora kupitia Kiswahili.

Nunua sasa kupitia www.mkukinanyota.com na @tphbookshop kwa sh. **60,000** tu.

# Diwani - CHUNGU TAMU (2)

**PITIO LA VITABU**

**DIWANI YA CHUNGU TAMU**

**MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI**

**WACHAPISHAJI: TPH**

**MWAKA: 1985**

***Inatoka toleo lililopita...***

Chatu amewakilisha wakoloni na kuku anawakilisha wananchi (Waafrika) walioonyonywa na kudhulumiwa na wakoloni. Mayai ya kuku yanawakilisha mali ghafi waliyodhulumu wakoloni kutoka hapa Afrika.

Katika shairi la"Chanzo ni Wenye Kauli" mwandishi anaonesha jinsi ulanguzi unavyosababisha dhuluma katika jamii. Mwandishi ameonesha kuwa chanzo cha ulanguzi ni upungufu wa bidhaa muhimu, tamaa, pamoja na uzembe toka kwenye vyombo vya dola. Ulanguzi husababisha rushwa, magendo na hivyo haki haitendeki katika jamii.

Mwandishi anasema;

"*Mianzo tukiijua,*

*Mipango tujipangia,*

*Kamwe pasiwe na njia,*

*Ulanguzi kurudia,*

*Iwe tu twahadithia,*

*Mithili historia".*

Katika shairi la "Kademokrasia Katoweka" mwandishi anasema;

*Ya msiba atayetamka,*

*Udikteta waja haraka,*

*Mtemi na walomzunguka,*

*Wawatia raia mashaka,*

*Dhuluma yatangazwa fanaka.*

Mwandishi anaonesha jinsi wananchi wanavyodhulumiwa demokrasia yao ya kutoa maoni yao hadharani. Demokrasia inapokosekana, dhuluma ya kutawala kwa mabavu huendelezwa.

Katika shairi la "Wengine Wabaki Taabuni", mwandishi anajadili juu ya dhuluma wanayoiendesha wakubwa dhidi ya watu wa tabaka la chini. Ameonesha kuwa majambazi wanayo idhini ya kufanya kila jambo kwa wanyonge, kwani hayo majambazi hulindwa na wakubwa. Anaendelea kueleza kuwa dhuluma inayoendeshwa na majambazi hapa nchini ni njama za walinzi *(vyombo vya dola).* Mwandishi Anasema;

*'Majambazi wanayo idhini,*

*Kufanya lijalo akilini,*

*Na hawataingia nguvuni,*


*Ma'na walinzi wamo njamani,*

*Tabu yaanzia kileleni."*

Mwandishi anaeleza kuwa tabu inaanzia kileleni maana yake ni tabu au dhuluma inaanzia kwa wakubwa. Hivyo ili tufanikishe suala la ujenzi wa jamii mpya ni lazima tujitoe mhanga kupambana na kila aina ya dhuluma katika jamii.

**2. KUFANYA KAZI KWA BIDII**

Uzembe na kutowajibika ni kikwazo kikubwa kinachokwamisha maendeleo ya jamii yoyote ile. Jamii yoyote ile yenye viongozi wazembe, viongozi wasiowajibika au wananchi wasiojua wajibu wao daima itabaki nyuma kimaendeleo. Mwandishi anaitaka jamii yetu ijue umuhimu wa kazi na kuwajibika katika suala zima




la maendeleo. Mashairi kadhaa katika diwani hii yanasisitiza kuhusu umuhimu wa kufanya kazi ili kuleta maendeleo ya jamii. Katika shairi la "Daktari askari". Mwandishi anasema;

*Saa moja jioni Landova inaingia,*

*Majeruhi sita na waganga pia,*

*Majeruhi vibaya wanalalama,*

*Waganga wao na sisi kazi tukaanza,*

*Hakuna kuamkiana au sijui nini.la,*

*Wagonjwa wengi misuli walikatika,*

*Wengine risasi walichimbiwa ,*

*Tukawekea damu,*

*Wa kushonwa,tukawashona,*

*Wakupasua ,tukapasua.*

**Itaendelea toleo lijalo...**



## ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UPATAZO

Ni mwezi wa kumi, u-hali gani ndugu na rafiki yangu? Sina shaka kuwa Mungu anaendelea kukupa pumzi na amani hata umelikamata jarida hili mpaka sasa.

Tukiwa tunaelekea kuumaliza mwaka, nikukumbushe tu kuwa mkanganyiko na msongo mwingi wa mawazo unaowakumba watu katika kipindi cha Mwezi Januari ni kutokana na kutokujiandaa kwa ile mikiki mikiki ya mahitaji katika mwezi ule. Wengi hushindwa kuhimili kipindi kile kwani huwa wametoka kwenye wakati wa sikukuu ya *Christmass*. Toleo lililopita pia nilikutaka ujiandae kutokana na matukio hayo ya kufungia mwaka yaani kipindi cha sikukuu ya *Christmass* na kipindi cha majukumu ya usomeshaji. Bora uwe na uonekane mwoga kuliko kuja kuonekana unashindwa kuhimili kuhudumia familia yako kiasi cha kuanza kulaumu watu kuwa hawakujali kwakuwa hawakusaidii au hawakukopeshi.

Tukiangazia mada yetu ya leo isemayo ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UPATAZO.

## ISHARA ZA KISAIKOLOJIA NI NINI?

Ishara za kisaikolojia ni alama ambazo huzalishwa kutokana na nguvu iliyopo ndani ya mtu, hizi ni nguvu asilia ambazo hazitokani na elimu ya darasani, huu ni uwezo wa mtu binafsi na uhai wa nguvu ya asilli ya ndani ya mwili, moyo na akilini mwa mtu husika. Kila mwanadamu anazo nguvu hizi ambazo zinaweza kumpa ishara mbalimbali katika maisha yake ya kila siku.

## ISHARA ZA KISAIKOLOJIA HUONEKANA KUPITIA NINI

Kuna watu wamebarikiwa nguvu kubwa ya asili ya maisha na mienendo yao kiasi cha kupelekea kupata ishara za mambo mbalimbali kupitia vyanzo mbalimbali vitokanavyo na mwili au fikra zao.

Haujawahi kuona au kusikia mtu akisema kuwa, “Mimi jicho la kushoto likinicheza najua msiba utatokea”, au ukasikia “mimi mdomo wa chini ukinicheza najua nitagombana”. Wengine nguvu zao za asili zimeenda mbali zaidi kwamba anaweza kupata maono au ndoto ya kitu na kweli kitu hicho kikatokea.

Saikolojia ni maisha yetu ya kila siku na matukio yake yanayotutokea. Wengi unaweza kuona au kusikia kuwa maisha yake yamevurugika kutokana na matatizo mbalimbali, kiuhalisia, ikiwa utaitumia nguvu ya asili uliyonayo katika kukulinda au kukutibia mambo yako basi hauwezi kupata tatizo lolote lile la kisaikolojia.

Ukichunguza nguvu zako za asili zinazokupa taarifa ya matukio yoyote yatakayotokea mbeleni ni wazi kuwa utajiepusha na maumivu yatakayokua yanakukuta. Sasa kama unajielewa kuwa jicho likicheza utapatwa na msiba, ukiona jicho linakucheza basi jiandae kwa msiba. Mkono umewasha jiandae kupata pesa. Elewa alama za matukio mbalimbali yatakayokutokea ili yanapoikutokea usiumizwe nayo moyoni.

**- SAIKOLOJIA -**

## ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UPATAZO

### UNAWEZAJE KUTUMIA ISHARA ZA MWILI?

Mungu ametupendelea nguvu za asili. Kila kiumbe kiitwacho binadamu Mungu amekitunuku tunu ya nguvu kubwa ambayo akiitumia kiukamilifu inaweza kumzalishia lolote lile alitakalo. Niliwahi kusema katika matoleo yaliyopita kuwa Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake, hivyo mwanadamu ni muumbaji msaidizi, ndiyo! Ni muumbaji msaidizi kwani baada ya uumbaji alimilikishwa kila kitu cha duniani akitawale. Ikawa alimilikishwa kila kitu hiyo itoshe kuutambua uwezo wa binadamu katika kufanya mambo yatokee.

Mwanadamu umepewa mamlaka na uwezo wa kuruhusu jambo au mambo yafanikiwe. Ikiwa nguvu yako ipo katika ndoto, kwamba ukiota ndoto zinatokea basi pia uwe na nguvu za kuruhusu zitokee au zisitokee. Kwamba umegundua kuwa jicho la kushoto likikucheza ni kweli msiba unatokea basi uonapo jicho limekucheza unayo nguvu ya kuruhusu msiba utokee au usitokee. Kwamba umegundua mkono wa kulia ukiwasha, we unapata hela na kupitiliza, basi mkono ukikuwasha unayo amri pia ya kupokea hela na ukaiamuru idumu na ukafanyia mambo yaliyo ya msingi.

Nguvu zote za uumbaji na utendekaji wa mambo yote yatokeayo ulimwenguni hivi sasa sio kwamba Mungu anayaumba upya, ni hiyo nguvu aliyowekewa mwanadamu ili kuwezesha mambo yakatokea. Ruhusu mambo chanya kutokea kupitia wewe. Mdomo umecheza, kwamba kwako hiyo ni ishara ya  kugombana basi sitisha kwa kutamka neno, wewe ni muumbaji msaidizi, muumbaji alitumia neno basi tamka neno kuidhinisha ishara za nguvu ya asili ulizooneshwa katika kufanya mambo yatokee.

Kwa wakati huu tuishie hapa hadi wakati ujao. Kwa mazungumzo na ushauri  wa kisaikolojia wasiliana nami kupitia namba hiyo hapo chini.

MADAM NEEMA MGAO

DODOMA

TANZANIA

0763013206.

### KISWAHILI CHAPITISHWA KUWA LUGHA RASMI YA KAZI UNESCO

Nyota ya Kiswahili imeendelea kuangaza Kimataifa baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuridhia Lugha hiyo kuwa moja ya Lugha rasmi zitakazotumika katika Mikutano Mikuu ya Shirika hilo. Hayo yamejiri Katika Mkutano Mkuu wa 43 wa Shirika hilo uliofanyika Samarkand - Uzbekistan kuanzia tarehe 30 Oktoba na utakaohitimishwa tarehe 13 Novemba 2025.

Tamko la UNESCO limetolewa leo Jumanne tarehe 11/11/2025. Kupitishwa kwa Kiswahili kumefuatia maombi yaliyowasilishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ushirikiano na Mabaraza ya Kiswahili BAKITA na BAKIZA.

Tanzania imepewa fursa ya kuwasilisha hotuba ya nchi baada ya maombi yake kuridhiwa ambayo ilitolewa na Mhe. Ali Jabiri Mwadini Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa na mwakilishi wa kudumu wa UNESCO.

Kupitishwa kwa Kiswahili kuwa Lugha ya kazi kunafanya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza yenye asili ya Afrika kupewa hadhi hiyo. Tukio hili maridhawa litafungua milango mingi ya Kiswahili katika taasisi, mashirika na Umoja wa Kikanda na Kimaifa.
Aidha, ikumbukwe kuwa, UNESCO Katika Mkutano wake wa 41 wa Novemba 2021 ndio uliopitisha azimio la kuwa na Siku ya Kiswahili Duniani ambayo huadhimishwa kila tarehe 7/7 na Siku hiyo ilitambuliwa rasmi na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa Julai,2024.

Hivyo basi, Kiswahili kwa sasa ni Lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusimi mwa Afrika ( SADC), Jumuiya ya Wazalishaji Almasi Afrika (ADPA) na Umoja wa Afrika (AU).

Nafasi hizi za Kiswahili Kimataifa zinategemewa kuimarisha ajira na fursa kwa wataalamu wa Kiswahili katika Ufundishaji, Tafsiri, Ukalimani, Uandishi wa Vitabu na Utangazaji. Ni azma ya Tanzania kukukuza diplomasia, shughuli za kiuchumi, uwekezaji, kilimo, utalii, madini viwanda na biashara kupitia lugha ya Kiswahili.
"Kidumu Kiswahili, Idumu Afrika".

# KITABU HIKI WAPASWA KUWA NACHO

MJUE MWANADAMU NA NGUVU ZILIZOMO NDANI YAKE

Ni kwa 15,000/= tu.

**MJUE MWANADAMU NA NGUVU ZILIZOMO NDANI YAKE**

**ISBN: 9789912429321**
**COSOTA: C0868882**

**BEI YA NAKALA HALISI TSH 15,000/= au kodisha kupitia online. Link na mawasiliano yapo chini**

Katika safari ya maisha, mwanadamu hujikuta akitafuta majibu ya maswali ya ndani kuhusu asili yake, uwezo wake, na nafasi yake katika ulimwengu. Kitabu hiki si tu muongozo wa kiroho, bali ni mwaliko wa kuangalia ndani ya nafsi, kugundua hazina iliyofichika na kuishi maisha yenye kusudio. Ni matumaini yangu kuwa kila ukurasa utakuwa mwanga mpya katika safari yako ya kiroho.

**MAWAZO NA HISIA**

Kwenye kurasa hizi utajifunza na kuelewa kwa kina jinsi mawazo yanavyoweza kuleta athari kubwa kwenye maisha yako. Utagundua kuwa kila kitu kinachoonekana chanzo chake ni mawazo na fikira tu. Lakini utaelewa kwa kina kuwa hisia zako ni sawa sawa na shamba lenye rutuba nzuri, hivyo linaweza kuotesha aina yoyote ya mbegu na kuvunwa kama mavuno bora. Hivyo, kile kinachoitwa hisia za huzuni au furaha ni matokeo ya mawazo yako mwenyewe. Hakuna anayeweza kukufundisha wewe kuwa na hisia nzuri, na hatimaye utagundua kuwa matendo yako ni matokeo tu ya mawazo na hisia zako.

**SIRI ZA NISHATI**

Katika sura ya pili, utajifunza na kuelewa kinaga ubaga kuhusu nguvu au nishati inavyoingia na kuanza kufanya kazi mwilini mwako. Sasa utaelewa kwa kina kuhusu miujiza na maajabu ya mwanadamu kuumba na kutengeneza dunia kupitia macho na moyo wake. Chakra ni vituo vya nishati; vituo hivi vinatumika kupokea na kusambaza nishati (prana). Binadamu ana vituo saba vya nishati, kuanzia root chakra mpaka crown chakra. Lakini pia binadamu ndani na nje ya mwili huu wa nyama ana miili sita mikubwa ambayo yenyewe ipo katika mfumo wa mwanga (subtle body). Hii ndiyo inasaidia kulisha na kutunza mwili wa nyama.

**KANUNI ZA MAUMBILE**

Utaendelea kusoma na kujifunza zaidi. Utajifunza kanuni za Mungu ambazo zinaongoza vitu na maumbo yote, ikiwemo maji, udongo, mimea, hewa, moto, na kila kitu. Hapa utajifunza kwa kina kanuni kama vile: kanuni ya umoja, kanuni ya chanzo na matokeo, kanuni ya mvuto, kanuni ya _kuwa-tenda-pata_, kanuni ya uwili, kanuni ya jinsia, na kadhalika.

Sasa utakua dereva mahiri ambaye anajua taratibu na sheria za barabarani. Sasa utaweza kuendesha maisha yako katika mwanga bora sana, kwa kuwa sasa utakuwa unafahamu kwamba kila kitu katika ulimwengu huu ni wewe mwenyewe. Chochote unachokifanya haufanyi kwa faida ya wengine bali kwa faida yako, kwa kuwa kila unachokiona ni taswira (reflection) ya wewe mwenyewe. Utagundua maisha ni kioo.

Utagundua kuwa kwenye maisha ni kuchagua muda na nafasi, kwa kuwa maisha ni mchezo mtakatifu unaotumia akili, hisia, na matendo.

**MAISHA NJE YA MWILI (ASTRAL TRAVEL)**

Utasoma mada za kutoka nje ya mwili, ndoto, na uchawi. Utajifunza jinsi ambavyo nishati inavyosafiri na kubadilisha maumbo kwa kutumia hiyo miili yako ya nje. Utaweza kugundua kuwa kumbe kinachotoka nje usiku ukiwa umelala huwa ni huo mwili wako wa tatu (astral body and astral travel). Na kitendo hicho si uchawi au maajabu kama ulivyoambiwa au kusikia, bali ni takwa la msingi sana la kimaumbile kama ilivyo kuingiza pumzi na kutoa pumzi nje. Kwa kuwa kitendo cha kupumua ni kitendo cha kiroho pia. Kupitia astral travel utakuja kugundua ugunduzi wote wa kisayansi na kitaaluma ulifanyika kupitia ndoto, na hicho kinachokuwa kinaota ni mwili wako wa tatu.

**MAPENZI NA NDOA**

Hapa utajifunza kwa kina na kuelewa siri za uumbaji wa ulimwengu ambazo asili yake ni tendo la ndoa. Kumbe nguvu ya sacral

chakra ndiyo asili ya kila kitu. Hapo utajua nguvu ya tendo la kujamiana katika kuleta mafanikio, utajiri, au kuleta uharibifu kwenye maisha yako. Utakuja kujifunza namna nzuri ya kuitumia nguvu hii katika ustawi wa maisha yako na jamii yako.

Utaweza kuwa mwangalifu sana kwenye kufanya mapenzi (sacred energy exchange/sex). Sio kitendo cha kiakili bali ni kitendo kitakatifu. Hauwezi tena kufanya sex kwa kujaribu au kwa sifa, kwa kuwa sasa unaelewa ni nini kilichomo ndani yake.

**TAHAJUDI (MEDITATION)**

Kwenye sura ya mwisho utajifunza tahajudi (meditation). Kwa kuwa sasa umeshajitambua wewe ni nani, hakika sasa wewe ni dereva mahiri. Dereva ambaye sasa unaweza kwenda kusoma mara kwa mara kupata ujuzi zaidi.

Meditation kwa lugha rahisi ni muunganiko wa nafsi yako na Muumba wako, kama ambavyo Yesu alisema "Mimi na Baba ni kitu kimoja," au kama ilivyo mbinguni na duniani. Imekuwa unapofanya meditation unawasiliana moja kwa moja na Muumba wako na hivyo kupata maarifa makubwa na busara za uumbaji moja kwa moja wewe mwenyewe, kwa kuwa wewe ni sehemu ya huo uumbaji.

Hapo utajifunza aina nyingi sana za meditation. Utaweza kujifunza meditation maalumu kwa ajili ya uchumi na fedha, meditation maalumu kwa ajili ya afya, meditation maalumu kwa ajili ya masomo, meditation maalumu kwa ajili ya ulinzi wa kiroho, meditation maalumu kwa ajili ya mahusiano, na kadhalika.

Nakualika tena usome kitabu hiki. Ni zaidi ya kitabu, hii ni njia ndogo inayomulika moyo wako na kukuongoza kwenye safari ya maisha.

**Bookshop na mawakala mbalimbali**

1. Elite book shops
Mbezi beach: 0753435484
2. University of dar es salaam: 0658780015

3. Palm village: 0767861151
4. Shoppers plaza: 076786151
5. Dodoma : 0745199860
6. Moshi Kilimanjaro: 0768954365
7. Tph Book Shop Mtaa wa Samora Posta: 0742556446
8. Kahama Shinyanga Phone: +255754056968
9. Kigoma Phone: +255620482945

Au wasiliana na mwandishi mwenyewe Chelestino Malinga 0754062900/ 0655062900. Pia waweza Soma online kupitia link hii hapa chini

https://lantern.co.tz/books/mjue-mwanadamu-nguvu-zilizomo-ndani-yake-9789912429321



## Kamba Za Frank Masai

Basi bwana.

Kuna siku nilipata ofa ya kuuza vitabu kama 20 kwa mteja wangu fulani hivi yupo huko Makumbusho. Nilikuwa namwona-ona mtandaoni lakini sikuwa nadhani kama atachukua nakala kwa mkupuo wa namna ile. Alikuwa ni jinsi ya kike, na kiukweli wanawake mnatusapoti sana waandishi kwa kununua vitabu vyetu. Mungu awatunze sana, bila nyie tungekuwa tunauza nakala 5. Na wanaume ahsanteni kwa sapoti yenu, sema hamuwashindi wakinamama.

Basi kwa kuwa nilikuwa nampelekea taita, ikabidi siku hiyo nivunje kabati afu funguo nikatupa. Niliamua kupendeza. Nikala shati la blue fulani hivi ya bahari *mixer* suruali nyeusi na koti la *dark blue*. Chini nikala 'moka' moja matata sana. niliinama pale Kimara Mwisho nikaokota kwa bei ya jioni. Kispray changu cha *cat walk* nika-psii-psii-psii, nikanukia *fresh*-marashi.

Mnyama mnyamwezi nikatoka *gheto* hata majirani waliacha kazi zao wakabaki wakinitazama mimi. Mkononi na begi lenye vitabu na mwondoko nikachenji nikawa kama sikanyagi ardhi. Kiukweli ungeniona, ungesema nimependeza kama Eminem anaenda kuchukua tuzo yake ya Grammy.

Mwamba huyo hadi kituo cha bodaboda hapa Kimara Golani. Toka hapo Golani hadi Suka huwaga wanasema bukujero ila mie huwa nakomaa naenda kwa buku. Sasa siku hiyo sikutaka kuwakomalia bei. Tayari dada mkubwa alikuwa kanijaza mapene. *Why* nililie buku angali nimelamba suti unyama.

Nikakwea boxer 101 na kumsihi dere' asongeshe tiritara. Sikutaka papara wala kakara maana vijana wetu hawa wakishapata double kick nusu, wanageuka Vin Diesel wa Fast and Furious. Suka akanielewa. Tukachukua uelekeo wa kukitafuta kituo cha daladala.

Dakika 10 nyingi, tukawa tumehitimisha safari yetu. Nikampa mwamba buku 2 afu kwa utulivu wa kisutisuti nikamwambia "*keep change boy*". Dere' akatabasamu wakati huo mie nanyata kitulivu na mkoba wangu wa vitabu kuliacha eneo lile na kuvuka hadi zinaposimama daladala.

Sasa bwana pale kituoni kulikuwa na pisi moja imenyooka sana. Pisi moja matata. Ndefu kiasi, white afu imekula super jeans ya blue iliyomkaa vema na kufanya shindu iliyojaza ionekane vema machoni mwangu. Itoshe kusema alikuwa na figa matata kinoma noma. Na kwa haraka niligundua ile ndio ndoto ya wanaume wengi, nikiwemo mimi maana kila aliyemwona, alimtazama japo kwa sekunde 5.

Nilisimama pembeni kwa utulivu wa maji ya baraka. Kibegi mkononi, saa na kacha vinashine kidizaini. Kutupa jicho pembeni nikaona yule dada ananitazama sana. Nami nikakaza kumtazama, tukawa tunatazamana. Ana macho makubwa, afu legevu. Too bad alikuwa anateseka na mafua. Basi yale macho kama yalikuwa yanataka kudondoka. Oya!

Tukaendelea kutazamana kwa muda huku kichwani nikijisemea mtoto kajaa kwenye mfumo wa Gamond, nikimkamata napiga 5. Hizo 5 sijui ni nini! Usinipe dhambi.

Huku na huku, Kule na Kule gari la Mbagala hilo. Lile kubwa kabisa. Nikaona manzi anawahi na kukwea. Mie safari yangu ilikuwa Makumbusho lakini nikasema potelea pwete, pisi imejaa vile niiache itembee, kwenye kikao mwisho wa mwaka ntasemaje? Nikaunga humohumo kwenye Mbagala State.

Nikakuta siti zimejaa lakini yeye kapata. Nikasema haina shanapa. Nitasimama na ataposhukia, na mie ntadondokea hapohapo halafu nitamtemea sound mchicha tembele kwa kwenda mbele mpaka amwage mchele.

Nazi ngumu ukivunja kwa ugoko tu, ikikutana na nondo inatii amri. Hii imani ilinipa ujasiri mkubwa na ushawishi wa kumtokea yule dada. Nilijua itakuwa tight kumpata lakini kwa maneno yangu, mtoto hatoboi hata dakika 1, atakuwa kaingia kwa Master Gamond. Atabweka mbona….

***Kamba za Frank Masai itaendelea toleo lijalo***

## SAKO KWA BAKO:

## KHADIJA ABDULLY: Fundi Nguo Asiyeacha Kusoma Vitabu

KATIKA matoleo ya nyuma ya Ngurumo ya Mwandishi, tumeendelea kuwatembelea wapenzi wa vitabu ambao ama wamejiajiri au wameajiriwa lakini bado vitabu havipo mbali na wao. Chapisho hili lilitoka mara ya kwanza kwenye Tokeo la XVI. Hapa tunalirudia.

Safari hii bado tunarandarada katika Jiji la maraha la Dar es salaam. Moja kwa moja mpka Mbagala tunakutana na mdau kindakindaki wa vitabu. Huyu hapa msikilize.

Naitwa Khadija Abdully, mimi ni mjasiriamali kwa upande wa ufundi nguo, au wengi wamezoe kuita fundi cherehani.



Khadija, katika pitapita zangu mtandaoni nimeona kuwa wewe ni mpenzi sana wa vitabu, nipo sahihi?

Upo sahihi, mimi ni mpenzi mzuri sana wa kusoma vitabu, majarida na machapisho mbalimbali.

Sasa, mi naona muda wote upo kwenye cherehani, muda wa kusoma unaupata kweli?

Muda upo kwa sababu huwa napangilia kazi zangu kwa uzuri na pia mimi muda mzuri zaidi wa kusoma huwa ni usiku.

Hongera sana. Watu wengi husema hawana muda wa kusoma vitabu au majarida au hapa hayo machapisho kwa kisingizio kwamba kazi nyingi, nachoka. Anyway, Khadija, vitabu vinakusaidia nini kwenye kazi yako?

Vitabu vinanijengea kujiamini na kupambana na vilevile vinanipa maarifa juu ya maisha kwa ujumla kwa sababu huwa nasoma aina mbalimbali ya vuitabu; kama vya mahusiano, maisha, biashara nk.

Kadiri ya kazi yako, unakutana na watu mbalimbali, wake kwa waume wakihitaji huduma hii. Je unatumiaje nafasi hiyo kuwahamasisha juu ya usomaji wa vitabu?

Yes! Mimi ukija ofisini kwangu lazima tu utakuta vitabu si chini ya vitatu, lakini mimi pia huwa napenda kushare na watu mbalimbali juu ya vitabu Fulani Fulani nilivyosoma.

Na kwa mwaka wa 2022 unaweza kutuambia umesoma vitabu vingapi?

Aisee kwa mwaka 2022 nimesoma vitabu vichache sana. Vingi nilivyosoma ni soft copy, kwa bahati mbaya siwezi kukumbuka idadi, vitabu kwangu huwa havikai jamani vinaazimishwa mno.

Wewe ni fundi nguo, au niseme fundi mitindo. Bila shaka unabuni mavazi, hebu tuanbie ni mtu gani maarufu umewahi kumbunia vazi?

Mimi bado sijafikia level ya ubunifu wa mavazi ingawa moja ya ndoto zangu ni kuwa mbunifu wa mavazi mbalimbali kwa wanamitindo, wasanii na watu wengineo pia.

Unawaambia nini Watanzania na wengine wote wanaokusoma sasa juu ya usomaji wa vitabu?

Nawashauri wajenge utamauni wa kusoma vitabu. Maarifa mengi sana yapo vitabuni, wawajemgee watoto pia watu wasiishie tu kusoma vitabu vya hadithi, kuna vitabu vya aina nyingi sana siku hizi. Mambo yamerahisishwa pia unaweza kusoma hata online.

Asante sana Bi. Khadija, sasa kama mtu anataka kuja kupata huduma ya kushonewa nguo, atakupataje?

Mimi napatikana Dar es salaam, Temeke, Mbagala Kuu. Wanaweza kunitafuta kwa mawasiliano yangu kwa njia ya Whatsapp 0627413637 na sms za kawaida ni 0654248614.

# MSALITI - 09

**Na. Richard Mwambe**



**Ilipoishia…**

**"Sijamuua ila nimemuacha kwenye hali mbaya sana," akajibu. Kituli akatikisa kichwa juu chini.**

**"Wapi?"**

**"Nilipomwacha?"**

**"Ndiyo!"**

**"Kulekule msituni, hakuna mtu atakayeweza kumuona…" Rodette akajibu, kisha akajiinamia kama mtu anayewaza jambo fulani.**

**"Sawa umefanya jambo zuri sana, nitatuma vijana wakammalizie…**

***Endelea...***

pah! Pah! Pah! risasi tatu tu za kichwa," Kituli akasema huku akiwa kakunja vidole vya mkono wake wa kuume mfano wa bastola na kufuatisha haya maneno 'Pah! Pah! Pah!'. Kauli ile ilimshtua kidogo Rodette lakini hakutaka kuonesha wazi. Ila pasi na kujua, Kituli aliligundua hilo. "Ukiwa hujafanya nilichokwambia, kati ya hizo risasi tatu, moja itazama kichwani mwako wewe," akamalizia kusema. Wawili hao walikutana ndani ya nyumba hiyo si kwa bahati mbaya, bali walikuwa katika kutekeleza mpango kabambe wa kutoa uhai wa mwanadamu. Tayari mioyo yao ilijawa ukatili na kusahau thamani ya uhai wa mwanadamu.

"Tutaondoka saa ngapi?" Rodette akauliza.

"Mpaka mwili wa yule mshenzi ufike hapa, ndo tutapanga kuondoka," akajibiwa.

"Basi mimi niwahi maana nin…" hakumaliza kusema kwani ganja jeusi la mkono wa Kituli lilimzuia kusema hilo atakalo.

"*No*! utabaki na mimi hapa!" ndilo neno lililofuata. Akachukua redio yake ndogo na kufungua kusikiliza taarifa ya habari. Kutoka eneo la Goma, redio nyingi zilikuwa zikitangaza kwa Lugha adhimu ya Kiswahili. Lugha namba nane ulimwenguni iliyotambuliwa na Shirika la Umoja la Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

*"Kutoka Dar es salaam Tanzania, miili kumi na sita ya wanajeshi waliouawa huko Congo imezikwa kwa heshima za kijeshi. Serikali kupitia kitengo maalumu cha jeshi la nchi hiyo imesema itaunda tume ya uchunguzi ili kujua chanzo halisi cha vifo hivyo…"*

"Aaahahahahahaaaa! Sisi ni bana ba Kongo…" Kituli alicheka kwa sauti na kujipigapiga kifuani akitamka maneno hayo. Rodette alibaki kimya akimwangalia. Moyoni mwake alijiuliza tu kuwa Kituli ni lipi hasa alikuwa akilifurahia. "Taarifa ya vifo vya wanajeshi wa Tanzania imenisikitisha sana…" akasema huku akiwasha sigara yake. "Hakuna jeshi zembe kama la Tanzania!" akaendelea kusema huku akimaliza kuiwasha ile sigara na kuvuta pafu mbili za haraka haraka.

"Zembe kivipi?" Rodette akauliza.

"Kivipi! Sasa we askari wote mnarundikana kwa sehemu moya, askari wa jeshi makumi mbili na sita, mnategemea nini mbele ya CRA, watu waliokula na kunywa damu, wenye mioyo isiyo na nyama wala huruma isiyohurumia mutu… CRA wakapiga wao vibaya na kuua yote, watushukuru sisi FARDC hata wakapata hiyo miili isiyo na kichwa," Kituli akazungumza. Rodette akabaki kimya bila kujibu lolote. Alijaribu kumtafakari huyo anayeongea hayo yote, hakutaka kukumbuka picha ile ya kuogofya jinsi watu wale walivyokufa.

Rodette ni mwanajeshi katika Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, 'FARDC'. Yeye kiasili alitokea mikoa ya Manyema ambako ilisadikiwa kuwa na wanawake wenye *shepu* za kibantu haswa. Basi, Rodette hakupewa sana wala hakunyimwa sana. Alikuwa mrembo kwelikweli ambaye kila rijali angetamani kulala naye kama si kumuoa kabisa. Akiwa ndani ya Jeshi hilo, viongozi wake wakaona kuwa mwanamke huyo anaweza kutumiwa kimkakati zaidi. Ama kuiba siri fulani kwa njia ya ulaghai wa mapenzi au kufanya jambo lolote lile la hatari ikiwemo kuondoa uhai wa mtu kwa kutumia uanamke wake. Aliweza, na alifanya ipaswavyo. Mara baada ya kuona majaribio ya kazi hiyo yamefanywa na mwanamke huyo kikamilifu kule Kinshasa basi viongozi wa Jeshi walikubaliana kumvua gwanda kisha kumpenyeza huko kwenye ardhi iliyojawa migogoro na mapigano yasiyokwisha kwa lengo moja tu, kuiba taarifa zozote zile hasa za majeshi ya nchi jirani au yale ambayo yapo kulinda amani chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa. Lakini si hapo tu bali alitumika hata miongoni mwa makamanda wa jeshi lenyewe la Kongo ili kupata taarifa hizo. Rodette kwa kazi yake tunamwita *'Honey Trap'* katika 'code' za kijasusi. Misheni nyingi alizotumwa alizifanikisha kwa asilimia kubwa. Na sasa alipewa kazi moja muhimu na ngumu sana dhidi ya Jenerali Mathurin Mampuya. Jenerali huyu alikuwa kinyume kabisa na sera

za wakuu wake dhidi ya mustakabali mzima wa kukomesha uasi huko Mashariki mwa nchi hiyo. Wakuu hao mbele ya jumuia ya kimataifa walijifanya kupambana na waasi, lakini kinyume chake walipanga mbinu na waasi haohao kuchimba na kubeba madini kisha kuyauza kwa nchi jirani hadi Ulaya. Biashara walioifanya ilikuwa na njia mbili ya malipo; ama wapokee fedha au wapokee silaha. Kikwazo pekee kwao ilikuwa ni Kamanda aliyekabidhiwa jukumu la kuongoza mapigano dhidi ya waasi hao katika mikoa ya Kivu, Beni, Goma na vitongoji vyake. Kamanda huyu alikuwa na mawazo tofauti. Hakuwa mchumia tumbo bali mpenda haki. Hiki ndicho kitu pekee kilichowafanya wakubwa wake kumweka mstari wa mbele ili afe. Rodette, mwanamke mrembo, mtamu kwa uzuri wake aliwekwa kama mtego na mwanaume huyo akanasa. Majaribio mawili ya kumuua Mathurin yaligonga ukuta. Hapo ndipo Rodette akaonekana kuwa turufu pekee. *Honey Trap!*

Saa moja baadaye mlango wa ile nyumba ndogo ukagongwa kwa fujo lakini kwa mpangilio maalum.

"Ingia!" Kituli akajibu na ule mlango ukafunguliwa. Wanaume wanne wakaingia wakiwa na bunduki aina ya AK47 vifuani pao.

"Hayupo!" yule mwanaume akasema huku wenzake wakiwa wamesimama nyuma yake. Kituli akageuka na kumtazama Rodette.

"Unanifanya mjinga siyo? Si unajua kazi uliyotakiwa uifanye ni nani alikutuma. Sasa utaenda kujibu kwake," Kituli akaongea kwa sauti kavu iliyojawa kila aina ya 'hakuna msamaha'. "Mchukueni huyu mwanamke, mpelekeni Ikelu, nakuja huko kesho," akawaambia wale wanaume. Wakamchukua Rodette na kutoka naye nje. Wakatokomea gizani.


❦

**NGARA-TANZANIA**

Ni Mji mdogo wenye kadiri ya watu wachache pia. Mji huu uliopeana mgongo na nchi ya Rwanda unakaliwa na watu jamii ya Wahangaza ambao wametapakaa hadi maeneo ya Biharamulo. Siku hii ilikuwa siku ya gulio. Mchangamano wa watu kutoka vijiji vya mbali ulikuwapo. Bidhaa mbalimbali kama vyakula vya mashambani, nguo, viatu na vingine kadha wa kadha viliuzwa. Kulikuwa na wachuuzi na wanunuzi. Wote walichangamana. Wengine walikuwa kutoka nchi jirani ya Rwanda ambao walivuka mpaka wa Rusumo na kuingia Tanzania. Kwa sababu walizoeleka na Askari wa hapa basi hata vibali hawakuwa navyo. Walivuka asubuhi na kurudi jioni.

Ni katika *Ngara Super Lodge,* Amata alipiga mbizi kwenye bwawa la kuogelea, na kufanya utundu wa kutosha wa kucheza na maji. Gina hakuwepo eneo lile isipokuwa mbele ya *Lodge* ile akitazama hekaheka za wapita njia katika barabara iliyo mita mia moja kutoka alipo. Gauni lake jepesi la hariri, lililopambwa kwa nakshi za maua ya kuvutia lilipepea kila lilipopigwa na upepo na kuacha sehemu kubwa ya miguu yake kuwa wazi. Kama jicho lako lilitaka kuona mapaja yake basi hilo lingekuwa jambo lako tu lakini juu ya magoti alivaa '*bana ngozi*' inayolandana rangi na ngozi yake. Kofia yake kubwa ya mzunguko ilikificha kichwa chake huku miwani nyeusi ikiyaziba macho yake. Aliendelea kuangaza huku na kule huku akifurahia hali ya hewa ya utulivu iliyolizunguka eneo hilo. Alipojiridhisha akatoka na kuliendea geti, kisha akatokomea mjini.

Gina alikata mitaa, akizunguka huku na kutokea kule. Akapita mtaa huu mpaka ule kule, yote hayo ilikuwa na kutaka kuijua mitaa hiyo. Aliulizia nyanya mara maparachichi. Na vichache alivyoona vinafaa kununuliwa alivinunua. Akatoka eneo lile na kuelekea mahali yalipoegeshwa magari ya kukodi.




Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

**MTUNZI: ASHA SIRAJ**
**Whatsapp 0789044345**



**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhila**

***Ilipoishia…***

**Namimi sikutaka kumvunja moyo nilimuahidi nitafanya vizuri na wala asiwaze kuhusu hilo.**
**Tuliendelea kuongea pale, aliniuliza kama nime-mmiss ila nilishikwa na aibu nikashindwa cha kumjibu zaidi ya kukaa kimya tu, aliniita zaidi ya mara mbili, "...mama sema tu kama umenimiss…"**

***Endelea...***

Jamani nilipokuwa nilihisi mwili wote unasisimka maana sikuwahi kuulizwa swali kama hilo.
Nimtazama *matron,* kwakuwa yeye alikuwa anasikia, aliniomba nimjibu.
"Ndio dokta unajua ukarimu wako unanifanya nione kuwa wewe ndiyo familia yangu tosha niliyobaki nayo".
Basi, *story* mbili-tatu, nilihofia sana mkuu asije akanikuta naongea na simu kwasababu haikuwa *weekend*. *Weekend* wanafunzi huwa wanaongea sana na wazazi wao na familia zao
Hata kabla *uncle* Jamari hajafariki weekend ndiyo siku ambayo nilikuwa napata kuongea naye sana.
Siku iliweza kupita na mtihani wa kawaida, tulifanya mitihani vizuri bila changamoto yoyote ile. Shule nyingi huwa zinaanza *graduation* kabla ya mtihani, ila sisi tulianza mtihani ndipo tukafuatia *graduation* yetu
Mambo yalikuwa bambam kama wimbo wa dj voice. Baada ya *graduation* hatukuwa na cha kufanya isipokuwa kila mmoja kurudi kwao.
Judithi ambaye ndiye rafiki yangu alikuja kuchukuliwa pale shule na mama yake mdogo. Nilimkumbatia na kumuaga rafiki yangu kipenzi, sijui kama nitaweza kuonana naye tena au ndo kama hivyo.
Mimi ndo nilibaki njia panda sijui ni wapi pa kwenda. Nilijawa na hofu sana, muda kidogo *matron* alikuja pale na kunikuta nipo kwenye hali tofauti sana, aliniomba nitulie maana hivyo ninavyowaza sio sahihi.
"Jamani *matron* kwani unajua ninachokiwaza?" nikamuuliza.
"Ndio Shazma, macho yako yanaonesha dhahiri kile ambacho unakiwaza, usijali kila kitu kipo sawa hivi punde utakuja kuchukuliwa".
"Matron! Nakuja kuchukuliwa na nani tena? Mbona sina taarifa za kuchukuliwa mimi hapa?" nikamuuliza kwa mashaka.
"Usijali, hivi punde utakuwa na furaha," akanijibu.

Nilihisi kama *matron* ananitia matumaini ya uongo. Kweli bwana, dakika chache liliwasili gari la Dokta Shahdu, ilinibidi nimuulize matron "Ni kwamba naenda kuishi na dokta au?"
"Shazma, mimi sijui ila ninachokijua mimi amekuja kukuchukua na sijui anakupeleka wapi," akanijibu.
"Hee! Wewe dada nisije kwenda kuchunwa ngozi," nikamjibu.
"Hahaaa!" alicheka sana *matron*. Mimi nikabaki kumtazama tu!
"We' cheka kama mazuri, unajua kabisa sijui uhalisia halisi wa maisha ya dokta" nikamjibu. "Naimani Mungu yupo na mimi," niliongea hivyo lakini *matron* muda wote alikuwa akinicheka. Sikujali kabisa.
Muda mchache nilipewa taarifa kwamba niandae vitu vyangu kwa ajili ya kuondoka. Nilishindwa nani nimuulize kuwa naenda wapi?
Hata *matron* aliyekuwa karibu yangu pia alikuwa akinicheka. Vyovyote vile sikujali, nilinyanyuka pale nikawa nimeenda kuchukua vitu vyangu bwenini kwa ajili ya kujiandaa na safari ambayo sikujua ni wapi napelekwa.

Nilitoa vyitu vyangu nje na muda kidogo Shahdu alikuja kunisaidia kubeba na kuvipeleka kwenye gari
Nilitamani kumuuliza ni wapi ananipeleka. *Matron* alikuja kunikumbatia pale huku akiniambia

"Kwa sasa maisha yako yatakuwa bora zaidi kuliko haya uliyokuwa unaishi hapa shule," alisema.
Sikuelewa amemanisha nini. Nilimuaga pale huku machozi yakinitiririka aliniomba nisilie kwasababu atakuwa akinipigia mara kwa mara kwa ajili yakuongea na mimi.
Shahdu alipanda kwenye gari nami nikiwa pembezoni mwake kwenye siti ya mbele.
"Shazma natumaini matokea yakitoka utakuwa kwenye kumi bora, aliongea Shahdu nikabaki kutabasamu tu pale
Nilijikaza ila mwisho wa siku niliamua kumuuliza ni wapi ananipeleka maana mimi nilitaka nirudi kwa shangazi niliamini huenda toka kifo cha mume wake labda atakuwa amejifunza kitu.
"Shahdu sihitaji kwenda pahala pengine zaidi ya kwenda kwa Shangazi Mariamu, siwezi kwenda sehemu nisiyoijua mimi, toka tumetoka shule naona unanizungusha tu hata tunapokwenda sipafahamu," nilimwambia.
"Shazma lini utaacha ubishi wako?" aliniuliza Shahdu. Nikashindwa cha kumjibu.
"Dokta Shahdu nipo chini ya miguu yako naomba nikamuone shangazi, walau likizo yote hiyo niwe kwake, anaweza akawa amebadilika," nikaomba.
"Unataka kwenda kwa shangazi, sindio?"
"Ndiyo dokta Shahdu, naomba unipeleke ni miaka minne sasa sijaonana naye hata kama amenifanyia unyama kiasi gani ule yule bado ni shangazi yangu," nikamjibu.
"Ohooo! Sawa naomba location ya kwenda huko kwa shangazi yako," akanambia kwa upole. Nilifurahi baada ya kuambiwa hivyo.


Haraka nilianza kumuelekeza, aligeuza gari na kuelekea barabara ya kinondoni. Alionekana kuwa kimya sana mpaka nikawa nahofia vipi kama kuna mabadiliko na hayuko tayari kunisomesha.
Nilijiuliza sana ila sikuwa na jibu, nilihisi presha ghafla kutokana na ukimya wake, nilimtazama sana ila hakujali aliendelea kuendesha gari kwa kasi sana hadi nikaanza kuogopa.
"Dokta Shahdu, ni kwamba umekasirika kwasababu nimekwambia nataka hii likizo yote niwe kwa shangazi?" nikamuuliza.
"Kwanini unaniuliza hivyo?" akanijibu kwa swali.
"Hapana dokta nimekuuliza kwasababu naona kama kuna kitu hakipo sawa ukimya wako unanifanya nihisi huenda ukawa umechukia mimi kukwambia vile" nikamweleza.
"Hahahaa!" alicheka kisha akageuka kunitazama, "unawaza kuhusu mimi?"
"Ndio dokta kwasababu wewe ndo msaada uliobaki kwenye maisha yangu hivyo naogopa kukukwaza, nasitaki kuwa chanzo cha wewe kukosa furaha," nikamwambia.
"Wala usijali Shazma ile ni familia yako una haki useme hivyo, na mimi sitaki kukuona ukiwa huna furaha kwa sababu yangu mimi. Kile utakachohitaji mimi nipo tayari nikupatie lakini sio kukuona ukiwa huna furaha".
Kiukweli dokta shahdu alikuwa na maneno matamu sana yani kama ulikuwa na hasira basi zote zitaisha kupitia maneno yake .

Tuliendelea na safari yetu ya kuelekea Kinondoni ila muda wote dokta Shahdu alikuwa anatabasamu huku *story* mbili tatu zikiendelea.

Baada ya robo saa kupita tayari tulikuwa tumewasili kwa shangazi. Nilishuka kwenye gari na kuelekea getini kwa ajili ya kugonga ili niweze kufunguliwa.
Nilianza kugonga na Dokta Shahdu naye alishuka kwenye gari akawa amenifuata pale getini.
Niligonga sana hadi nikachoka mkono, ila sauti ya Munira ilisikika kwa mbali akiwa anadai kuwa anakuja. Nilianza kufurahi kabla hata sijamuona dada yangu, nilikuwa nimemmiss sana. Nimiaka mingi sasa hatujaonana.
Nilihisi kama anachelewa kufungua mlango maana nilitamani nimkumbatie kwa zile furaha nilizokuwa nazo.

Geti lilifunguliwa na kweli alikuwa Munira nilimsogelea nakumuwawo. "Khaa! Kwani we vipi kunukishana kikwapa sa'hivi," aliongea hivyo Munira hadi pozi likaniishia. Niligeuka nakumtazama Shahdu aliyebaki kashikilia mdomo kutokana na yale naneno ya Munira.

*Itaendelea ...*




***ITAENDELEA....***

# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (22)

***Ilipoishia…***

**Asubuhi iliyofuata, Alibaba aliamka mapema sana, akachukua makapu sita na kuyafunga kwa wale punda wake watatu. Kisha akaiaga familia yake na kuelekea msituni.**

***Endelea...***

Alipofika katika jiwe kubwa la lile pango, alisimama na kuangalia maeneo yaliyozungula pango lile. Aliuona mti mrefu ambao alijificha mara ya kwanza alipogundua pango lile. Alisikiliza kwa makini sana – hakukuwa na sauti za kwato za farasi, wala sauti za wanyama wa porini, hakusikia wala kuona chochote ambacho kingemtia hofu.

Akavuta pumzi nyingi ndani na kusogea karibu na jiwe kubwa la lile pango. Kisha aksema lile neno la siri, "Fungukaaaa sesmiiiii!!!!"

Taratibu kabisa, lango likafunguka na Alibaba akaingia ndani. Akaona sehemu ambayo aliuona mwili wa kaka yake. Alibaba aligeuka haraka sana ili asipatazame sana mahali pale kwani kungemtia huzuni zaidi. Akaendelea kwenda ndani zaidi.

Pango bado lilikuwa na hazina nyingi sana, dhahabu, fedha, sarafu, pete, bilauri za rangi ya fedha na hazina nyingi zaidi ya hizo – kitu ambacho hakukiona pale ni vitambaa vya hariri.

Alibaba akafikiri kidogo.

"Khoja Hussein!" alijisemea moyoni. "Kiongozi wa wezi alijifanya mfanya biashara mkubwa wa vitambaa vya hariri na kufanya urafiki na mwanangu! Alijaza duka vitambaa vya hariri – kumbe vilitoka humu pangoni."

Alibaba akaendelea kuangalia hazina zote.

"Hakuna mtu aliyekuwepo humu kwa muda mrefu sana," Alijisemea. "Nafikiri wezi wote wameshakufa. Hazina hii yote ni yangu!"

Hivyo basi, akachukua baadhi ya mifuko ya sarafu za dhahabu, na baadhi ya vito pamoja na bilauri nzuri zenye kung'aa.

"Hizi bilauri zitapendeza sana zikiwa mezani kwetu." Alifikiri. "Mke wangu atazipenda sana."

Alibaba akazibeba hazina hizo alizokusanya na kuzijaza katika makapu yake sita yaliyobebwa na punda wake.

"Hii inatosha kwa sasa," alijisemea. "Sitaki kuwa mroho sana."

Kisha katoka nje ya pango na kusema neno la siri, "Fungaaaaa sesmiii!!"

Jiwe kubwa likajifunga na likaonekana kama mawe mengine tu ya pale msituni.

Wakati jua linakaribia kuzama, na mbingu inabadilika rangi na kuwa kama zambarau iliyokoza, Alibaba na punda wake wakaondoka kurudi nyumbani.

Hazina iliyochukuliwa na Alibaba ilidumu kwa mwaka mwingine zaidi. Wakati huu, Marjane na Khalid walipata mtoto wa kiume na Alibaba akaamua kumpa Khalid siri ya lile pango.

"Wewe ni baba sasa, Khalid," Alibaba alimwambia mwanae. "Kuna kitu nataka kukuonesha – kitu muhimu sana. Unajua kwamba nina dhahabu, na unajua kwamba nilizipata kutoka kwa kundi lile la wezi. Wale waliokuwa wanataka kuniua."

"Ndio baba," Khalid alijibu. "Marjane wangu mwerevu aliwaua! Na ninajua kwamba dhahabu zile ndizo zilizokutajirisha."

"Ndio, haswaa!!" Alibaba alisema. "Lakini sasa, nimezitumia nyingi sana, na sasa nahitaji nyingine zaidi. Nataka nikupeleke kwenye pango ambalo dhahabu hizo zinapatikana, Khalid. Siku moja wewe au mwanao mnaweza kuhitaji kujua mahala zilipo."

"Ahsante sana, baba," Khalid alijibu. "Nina furaha kwa kuniambia hivyo. Nilikuwa nashangaa hizi dhahabu mahali zinapotoka."

Siku iliyofuata, Alibaba na mwanae wakafunga safari ya kuelekea msituni na walienda na punda wao watatu.

Kisha Alibaba akasema neno la siri, "Funguaaaa sesmiiii!!!"

Lango likafunguka, kisha Alibaba na mwanae wakaingia ndani.

Pango bado lilikuwa na hazina nyingi sana. Dhahabu zote pamoja na fedha na vito mbalimbali vilikuwa vinang'aa kutokana na mwanga unaoingia pangoni kupitia vitundu vya juu ya pango hilo. Khalid aliduwaa sana kuona hivyo.

"Siamini macho yangu!" alisema. "Kuna hazina nyingi sana!"

"Hakuna mtu aliyeingia humu kwa mwaka mzima sasa," alisema Alibaba huku akiangalia maeneo yote ya pangoni mle. "Tutakuwa salama kabisa."

Wakachukua baadhi ya hazina na kujaza kapu zao na kurudi nyumbani.

"Ahsante kwa kuniambia siri yako, baba," Alisema Khalid wakati wanarudi nyumbani. "Mwanangu akiwa mkubwa, nitamwambia pia kuhusu hazina zile na nitampeleka huko pangoni."

Alibaba alicheka kwa furaha. "Ndiyo," alijibu. "Na yeye pia atamwambia mwanae."

Familia ya Alibaba iliishi kwa amani na hawakuwa masikini tena.

*MWISHO*

# TUZO YA NOBEL YA FASIHI 2025

Na Mwandishi wetu.

László Krasznahorkai, mwandishi kutoka Hungary, ameshinda Tuzo ya Nobel ya Fasihi 2025 kwa kazi zake zenye “mvuto wa kipekee na maono makubwa ambayo, katikati ya hofu ya maangamizi, zinathibitisha tena nguvu ya sanaa”. Alitangazwa mshindi tarehe 9 Oktoba 2025, akiwa Mhungaria wa pili kushinda tuzo hiyo baada ya *Imre Kertész* (2002). Taarifa rasmi ilitolewa na Academy ya Kiswidi kupitia tovuti ya nobelprize.org.

**2. Wasifu na Historia Fupi**

László Krasznahorkai alizaliwa tarehe 5 Januari 1954, mjini *Gyula*, Hungary. Alikulia katika kipindi cha utawala wa kikomunisti nchini Hungary, hali iliyompa mtazamo wa kipekee kuhusu kuporomoka kwa mifumo ya kijamii na kisiasa, jambo linalojitokeza sana katika kazi zake. Baadaye alisafiri sana, hasa kuelekea Asia ya Mashariki, na utamaduni wa eneo hilo uliathiri kwa kiasi kikubwa maandiko yake ya baadaye.

**3. Mtindo, Kauli Mbiu na Umuhimu wa Kazi Zake**

Krasznahorkai ni mwandishi anayejulikana kwa:

Uandishi mzito, wa kifalsafa na wa kiapokaliptiki – akichunguza maisha ya kisasa, upweke wa mwanadamu, na utafutaji wa maana ya uwepo.

Sentensi ndefu sana na kurasa chache zenye mapumziko – mara nyingine sura nzima huwa ni aya moja tu, jambo linalounda mtiririko wa maandiko unaovutia na wenye nguvu ya kipekee.

Kauli kuu katika kazi zake ni kuporomoka kwa mifumo ya kijamii au kisiasa, upotevu wa matumaini, na ubinadamu unaojikokota katikati ya machafuko.
Kamati ya Nobel ilisema: *“Ni mwandishi mkubwa wa hadithi za kifasihi wa Ulaya ya Kati katika jadi ya Kafka na Thomas Bernhard, mwenye upeo wa kiajabu na ucheshi wa kiza.”*

**Kazi Maarufu**
Baadhi ya vitabu vyake vinavyotambulika duniani ni:

**Satantango** iliyoandikwa mwaka 1985 – Riwaya iliyompatia umaarufu, kuhusu kijiji cha wakulima waliotelekezwa, wakisubiri “muujiza” usiotokea.

**The Melancholy of Resistance** iliyoandikwa mwaka 1989 – Riwaya ya kidhahania kuhusu upinzani, kuporomoka, na upuuzi wa mifumo ya binadamu.

**War and War** iliyoandikwa 1999 – Inachunguza ndoto za kutoroka, uzito wa historia, na utafutaji wa maana katika ulimwengu usio na mwelekeo.

Baadhi ya kazi zake zilibadilishwa kuwa filamu na mtayarishaji maarufu *Béla Tarr* (mfano *Satantango* na *Werckmeister Harmonies*).



László Krasznahorkai—mshindi wa Tuzo ya Nobel katika fasihi 2025

# HISTORIA YA VITABU ULIMWENGUNI—8

## HISTORIA YA KITABU – THE DIVINE COMEDY

**Mwandishi:** *Dante Alighieri* (1265–1321)
**Asili:** Firenze (Florence), Italia
**Mwaka wa uandishi:** Karibu mwaka 1308 hadi kifo chake 1321
**Lugha:** Kiitaliano cha zamani (*Tuscan dialect*)

### Asili na mazingira ya uandishi

Wakati Dante anaandika kazi hii, alikuwa amefukuzwa kutoka mji wa Florence kwa sababu ya migogoro ya kisiasa kati ya makundi ya *White Guelphs* na *Black Guelphs*. Uhamisho huu ulimuumiza sana—kimaisha na kiroho.
Katika hali hiyo ya maumivu, upweke, na tafakuri ya maisha, Dante akaandika *The Divine Comedy* kama safari ya roho kuelekea kwa Mungu—kutoka giza la dhambi, kupitia toba, hadi nuru ya neema.

Aliita "*Commedia*" (yaani "**Comedy**") kwa sababu ina mwisho wa furaha (Dante anafika mbinguni). Neno "Divine" (yaani "-a Kiungu") liliongezwa baadaye na wachapishaji.

## MUHTASARI WA KITABU

Kitabu hiki kina sehemu tatu:

### Inferno (Kuzimu)

Dante anaamka akiwa amepotea kwenye msitu wa giza, ishara ya dhambi na machafuko ya maisha ya kibinadamu.
Anaongozwa na Virgil, roho ya mshairi wa Kirumi, ambaye anampeleka kupitia mizunguko tisa ya kuzimu.
Kila mzunguko una adhabu maalum kwa dhambi fulani – kwa mfano, wazinzi wanapeperushwa na upepo mkali, waongo wanaungua, na wasaliti wako kwenye barafu.

**Mafundisho:** Dhambi ina matokeo. Haki ya Mungu inahakikisha kila tendo lina matokeo yake.

### Purgatorio (Toharani)

Baada ya kutoka kuzimu, Dante anapanda mlima wa toharani. Hapa roho zinatakaswa kutokana na makosa yao kabla ya kuingia peponi.
Safari hii inaonesha nguvu ya toba, maombi, na neema ya Mungu.

**Mafundisho:** Mtu anaweza kubadilika. Toba ya kweli inafungua mlango wa wokovu.

### Paradiso (Peponi)

Hapa Dante anaongozwa na Beatrice, mwanamke anayewakilisha hekima na upendo wa Mungu.
Anaingia Mbinguni na kuona ngazi za heri, akishuhudia uzuri na utukufu wa Mungu.
Safari yake inaishia kwa kuona mwanga wa milele — ishara ya umoja na Mungu.

**Mafundisho:** Upendo wa Mungu ndio nguvu kuu ya ulimwengu; ni mwisho wa safari ya roho.

## MAFUNDISHO MAKUU YA KITABU

1. **Maisha ni safari ya kiroho.** Kila mtu anasafiri kutoka giza la dhambi kuelekea nuru ya Mungu.
2. **Dhambi huleta mateso, toba huleta uhuru.** Dante anatuonya kwamba kila dhambi ina matokeo, lakini rehema ipo kwa wenye kutubu.
3. **Mungu ni haki na rehema.** Haki ya Mungu inaonekana kuzimuni, rehema yake toharani, na upendo wake peponi.
4. **Upendo wa kweli ni wa kiroho.** Uhusiano wa Dante na Beatrice unaonyesha kwamba upendo safi unamvuta mtu karibu na Mungu.
5. **Kila mwanadamu ana nafasi ya wokovu.** Hata walioanguka wanaweza kuinuka kwa imani, maombi, na matendo mema.

## UMUHIMU WA KAZI HII

- Ni **nguzo ya fasihi ya dunia ya Magharibi**, ikilinganishwa na *Iliad*, *Odyssey*, na *Bible*.
- Iliweka msingi wa **lugha ya Kiitaliano sanifu**.
- Inabeba mafunzo ya **imani, falsafa, siasa, na maadili**.

**Ni mfano wa sanaa ya kubadilisha mateso ya kibinafsi kuwa fumbo la kiroho la ulimwengu wote**.

# KITABU NILICHOSOMA

## MENO YA MBWA

**NILIYOYAPATA KITABUNI**

**Maktaba:**
Anna Mbise Pan African Mobile Library

**Jina la Kitabu :**
Meno ya Mbwa

**Mwandishi:**
Kalmas Konzo

**Msomaji:**
Shaib Salim Idrak

**Mwezi wa Usomaji:** Agosti 2025

Kitabu kinaelezea jinsi maisha ya wanajamii yanavyoweza kubadilika kw sababu ya tabia zisizofaa. Mfano, familia zinavyoweza kuingia matatizoni kwa sababu ya ubinafsi wa nafsi. Wazazi wa familia wakikosa uadilifu na uaminifu ndiye wanakuwa maadui namba moja wa familia.


Haya ni baadhi ya madhumuni ya mwandishi kuhusu cha kitabu cha Meno ya Mbwa.

**1. Ubinafsi.**
Mzee Ngudu hakujali hisia za mke wake, alijali matamanio yake ya nafsi, kutembea na wanawake wengine nje ya ndoa yake, ikiwa tabia hiyo ndio ilisababisha familia yake kupata matatizo hadi akaitelekeza.

**2. Maisha yana sura nyingi.**
Tumeona maisha aliyokuwa akiishi veneranda akiwa wazazi wake za damu, alipofariki mama ake veneranda, akaletwa rose, mama wa kambo wa veneranda, maisha yakabadilika, hadi kupelekea kubwa mtoto wa mtaani, kisha kupewa hisani na mama mwema.

**3. Tamaa si nzuri.**
Mama yake samantha(rose) tamaa ya mali ilimfanya afanye uuwaji kwa mama veneranda ili aolewe yeye na awe mrithi wa mali za mzee Ngudu. Alifanikiwa kupata mali ila hazikudumu, sababu mali ya dhuruma haidumu.

**4.Malezi bora ni tunu kwa mtoto.**
Muandishi ametuoneah malezi aliyopewa samantha na mama yake hayakuwa mazuri, alishindwa kutumia njia nzuri za kupambana na changamoto zilizomkabili yeye na mama yake. ikafikia hatua akawa mwizi ili apambane na changamoto za maradhi ya mama yake.




**5.Kusamehe na kuishi kw upendo.**
Mwandishi kumuelezea veneranda, jinsi alivyonyanyaswa na mama yake wa kambo na Samantha, ila aliwasamehe wote na kuishi nao tena kw upendo, sababu makosa umefanya mtu kuwa bora.



# HABARI PICHA





BongoPoly mchezo uliochezwa kwenye tukio la kalamu Salamu pale Alliance Francaise, Dar es sakaam





Washiriki wa Kalamu Salamu wakitoa maoni yao katika tukio hilo.






**Wajumbe wa Mkutano wa UNESCO uliopitisha Lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kikazi.**

**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

## NCHI YANGU TANZANIA

Chozi linanidondoka, huzuni nyingi moyoni
Moyo wangu unachoka, zabaki kwikwi rohoni
Wapi mnatupeleka, hatuelewi jamani
Nchi yangu Tanzania, itunze yako amani.

Tuliyonayo amani, wazee metuachia
Tuitunzeni jamani, kabla tujaijutia
Tuelekee mezani, mambo kuzungumzia
Nchi yangu Tanzania, itunze yako amani.

Viongozi wetu pia, hebu jitafakarini
Damu yatumwagikia, maiti zi mkononi
Kila tukifikiria, kesho yetu tuioni
Nchi yangu Tanzania, itunze yako amani

Itunze yako amani, nchi yangu Tanzania
Tuone yake thamani, tusije kuililia
Wanasiasa jamani, twawataka kusikia
Nchi yangu Tanzania, itunze yako amani

Roho zimeteketea, kila nyumba wanalia
Nguvu kazi mepotea, kudai demokrasia
Hii imepelea, makovu kutuachia
Nchi yangu Tanzania, itunze yako amani.

Sikia Mama Samia, Raisi wetu makini
Wanao twakulilia, rudisha utu nchini
Sote tuwe familia, kama ilivyo zamani
Nchi yangu Tanzania, itunze yako amani

Moyo wangu waumia, tamati napofikia
Kila nikifikiria, machozi yananijia
Wanasiasa sikia, damu itawalilia
Nchi yangu Tanzania, itunze yako amani.

**03 Oktoba, 2025**
**Ichenjezya, Vwawa, Mbeya**

## GEN Z

Gen Z tulieni
Upya tafakarini
Vurugu kwetu za nini
Na kupoteza amani?

Gen Z tulieni
Jambo wekeni mezani
Hoja mzitungeni
Ziwafike kilingeni

Haki sote twadai
Wakaguru kwa wamasai
Lakini vurugu hazifai
Hayo siyo madai

Tufanye maandamano
Kwa sheria tangamano
Nani atasema no
Kwa amani mshikamano?

Mevunja za watu mali
Mmeiba nyingi mali
Hiyo si halali
Amani hatuijali

Sote twahuzunikia
Haya yaliyotokea
Yatubidi jifunzia
Kamwe kutoyarudia

Vijana tunza amani
Kwani tutaitamani
Mabadiliko makini
Tuyapate kwa amani.

Tulinde amani yetu vijana wa tanzania,.

***Shujaa Maneno***
***Bagamoyo Pwani***

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# TANGAZO


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya Riwaya
Kinondoni Morocco
Simu:
0655428085
Zammira


KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
MSALITI
15,000/=
Kona ya Riwaya
BOOKSHOP
Fika dukani kwetu au wasiliana nasi Kwa Simu
0655 428 085
Mliopo mikoani tunakutumieni.


KINAPATIKANA
ARUSHA
Kinapatikana Kwa Ally Said Shaban, nje tu ya KIMAHAMA Bookshop
Simu: 0757690302 na 0656744390
KAMANDA AMATA
MSALITI
15,000/= tu
Jipatie Nakala Yako Sasa!


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
ARUSHA
Nje ya Duka KIMAHAMA
Simu
+255 757 690 302
ALLY SAID

# MWANDISHI WA ENZI HIZO: 1. DADI MTIKA MWAWARE

Dadi Mtika Mwaware au hujulikana kama 'Dadi Mwaware' ni mwandishi wa Kiswahili ambaye ameandika vitabu vya riwaya za hadithi za kusisimua.

Huyu ni mmoja wa waandishi aliyetamba kiuandishi miaka ya 1970 mpaka 1980. Sikuweza kupata maelezo kuhusu maisha yake kiujumla kutokana na ufinyu wa taarifa.

Labda sasa tumfahamu kupitia kazi zake za kifasihi, lakini kama kuna msomaji anayejua taarifa zaidi za mwandishi huyu basi awasiliane nasi ili tumjue zaidi.

Lakini anaorodheshwa katika orodha ya waandishi wa Kiswahili kama mmoja wa wale walioandika riwaya za kusisimua 'Thriller'

Dadi Mtika Mwaware ameandika vitabu riwaya mbili zinazojulikana sana na wasomaji wa enzi za miaka ya 1970 mpaka 1980.

1. **OPERESHENI VIPUSA (1977**

Riwaya hii imeandikwa mwaka 1977 na kuchapwa na Black Star Agencies mwaka huohuo 1977

Muhtasari wa riwaya hiyo: Ni riwaya ya kusisimua 'Thriller' inayosimulia Siasa za uhalifu. Inaelezea juu ya ufisadi na biashara haramu ya ujangili.

Inasimulia kuhusu mkuu wa polisi katika Mkoa wa Mtwara anayehusika katika udanganyifu na usafirishaji wa pembe za ndovu na kiboko (vipusa). Hadithi hii inahadithia jinsi wizi na ufisadi vinavyogusa vyombo vya dola na jamii.

**Msimamo wa Kitabu katika fasihi:**

Kinaonekana kama mfano wa riwaya za "operesheni/uchunguzi" za Kiswahili za karne ya ishirini ambazo zilichambua uhalifu wa rasilimali (wildlife trafficking) na matumizi mabaya ya madaraaka.

2. **MAPUTO / NTEKO VANO MAPUTO (1980)**

Riwaya hii imeandikwa na kuchapwa mwaka 1980 kupitia mchapishaji Longman Tanzania. Ina kurasa 193.


**Muhtasari wa riwaya:** Hii ni riwaya nyingine ya kusisimua 'thriller'. Hadithi kuu inasimulia juu ya uhalifu mkubwa wa wizi wa dhahabu na biashara haramu na uhusiano wa wahalifu na miundombinu ya kitaifa/kimataifa.

**Upatikanaji wa vitabu hivi**

Kiukweli katika uchunguzi uliofanyika imeonekana wazi kuwa kwa sasa vitabu vya mwandishi huyu havipatikani kabisa madukani isipokuwa kwa watu wachache ambao wanavimiliki tangu miaka hiyo.

Lakini kwa mtu yeyote anayetaka kusoma vitabu hivi labda atembelee Maktaba Kuu ya Taifa na kutaja majina hayo, yaani; Operesheni Vipusa au Maputo Nteko Vano bila kusahau jina la Mwandishi Dadi Mtika Mwaware.

Lakini safu hii ya Kutoka Maktaba inaomba mtu yeyote mwenye taarifa zaidi za mwandishi huyu awasiliane nasi ili tuweze kumtambulisha kwa wasomaji wa kizazi cha sasa kupitia jarida hili.



# ELIMU JAMII

## SAFARI YA MALEZI 6: TEKNOLOJIA NA MALEZI

5.0 **TEKNOLOJIA NA MALEZI**
Katika dunia ya sasa inayotawaliwa na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, maisha ya binadamu yamebadilika kwa kiasi kikubwa. Watoto wa leo wanalelewa katika mazingira yanayozungukwa na vifaa vingi vya kielektroniki kama simu janja, kompyuta, runinga na intaneti. Mabadiliko haya yameathiri kwa namna kubwa jinsi wazazi, walimu na walezi wanavyowalea watoto wao.

Kwa upande mmoja, teknolojia imekuwa msaada mkubwa katika kurahisisha malezi na elimu ya watoto. Hata hivyo, kwa upande mwingine, matumizi mabaya ya teknolojia yameleta changamoto zinazoweza kudhoofisha malezi bora. Hivyo basi, sura hii itajadili umuhimu wa teknolojia katika malezi, athari hasi za matumizi yake, na wajibu wa wazazi, walimu na jamii katika kuhakikisha teknolojia inatumika kwa njia chanya.

5.1 Umuhimu wa Teknolojia katika Malezi
Teknolojia imechangia kwa kiwango kikubwa katika kuboresha malezi ya watoto, hasa inapotumika kwa njia sahihi. Mchango wake unaonekana katika nyanja za elimu, maadili, na ujenzi wa stadi mbalimbali za maisha.

Na. KELVIN JOHN KYARA

0753767930

Kwanza, teknolojia imerahisisha upatikanaji wa maarifa. Wazazi na walimu wanaweza kutumia mitandao ya kijamii, video za mafunzo, na programu za simu kuwafundisha watoto elimu, maadili na stadi za maisha. Kwa mfano, kupitia majukwaa kama YouTube, watoto wanaweza kujifunza masomo ya darasani na elimu ya maisha kwa urahisi zaidi. Hii husaidia kupanua upeo wa maarifa yao na kuongeza ubunifu.

Pili, teknolojia imeboresha mawasiliano kati ya wazazi na watoto. Wazazi wanaweza kuwasiliana kwa urahisi na watoto wao wanapokuwa mbali kwa sababu za kikazi au shughuli nyingine muhimu. Hivyo, husaidia kudumisha ukaribu na kufuatilia maendeleo ya watoto wao.

Tatu, teknolojia inasaidia katika kukuza uelewa wa dunia na maadili mema. Kupitia michezo ya kielimu, filamu za maadili na mafundisho ya dini yanayopatikana mtandaoni, watoto hujifunza tabia njema, nidhamu na mtazamo chanya kuhusu maisha. Kwa njia hii, teknolojia inakuwa chombo muhimu cha kujenga utu bora wa mtoto.

**5.2 Athari Hasi za Teknolojia katika Malezi**
Pamoja na faida zake, teknolojia imeambatana na changamoto ambazo, endapo hazitadhibitiwa, zinaweza kudhoofisha malezi bora. Watoto wengi hutumia muda mwingi kwenye runinga, simu au michezo ya mtandaoni kuliko kuzungumza na wazazi wao. Hali hii hupunguza mawasiliano ya ana kwa ana, na hivyo wazazi hushindwa kufuatilia mienendo na maendeleo ya watoto wao kwa ukaribu.

Aidha, maudhui mengi yanayopatikana mtandaoni hayana maadili. Baadhi ya katuni na video zinaweza kuwa na ujumbe usiofaa na kuwapotosha watoto kimaadili na kitabia. Bila uangalizi wa wazazi, watoto wanaweza kuiga tabia hizo na kuathiriwa kisaikolojia na kijamii.

Matumizi kupita kiasi ya teknolojia pia yamechangia kuongezeka kwa uraibu wa simu na michezo ya mtandaoni, hali inayosababisha watoto wengi kuwa wapweke, wasio na umakini shuleni, na kupoteza ari ya kujifunza. Zaidi ya hayo, wazazi wengi wamepunguza muda wa kuwasiliana na watoto wao kwa sababu wao wenyewe wamekuwa wakitumia muda mwingi kwenye runinga au mitandao ya kijamii. Hii inavuruga uhusiano wa kifamilia na kudhoofisha malezi.

5.3 Majukumu ya Wazazi, Walezi na Jamii
Wazazi, walezi na jamii kwa ujumla wana jukumu kubwa kuhakikisha teknolojia inatumika kwa manufaa katika malezi ya watoto.

Kwanza, ni muhimu kudhibiti muda wa matumizi ya vifaa vya kidijitali. Wazazi hawapaswi kuwaacha watoto kutumia simu, kompyuta au runinga muda wote. Badala yake, wanapaswa kuweka ratiba maalum ya matumizi na kuhakikisha wanawasimamia watoto wakati wa kutumia vifaa hivyo.

Pili, ni lazima watoto waelimishwe kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia. Wazazi na walimu wanapaswa kuwafundisha watoto kutambua tofauti kati ya maudhui mazuri na mabaya, na kuelewa umuhimu wa kutumia teknolojia kwa ajili ya elimu na ubunifu.

Tatu, wazazi na walezi wanapaswa kuwa vielelezo bora kwa watoto wao. Mzazi anayekaa muda wote akitumia simu mbele ya watoto anaweza kuwasababisha nao kuiga tabia hiyo. Watoto hujifunza zaidi kwa kuiga, hivyo ni muhimu wazazi kuonyesha mfano wa matumizi yenye nidhamu na manufaa.

Aidha, jamii kwa ujumla inapaswa kuhimiza matumizi ya teknolojia yenye maudhui chanya. Ni vyema kuanzisha programu rafiki kwa familia, majukwaa ya kijamii yanayokuza maadili, na mifumo inayowezesha wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto katika elimu na afya.

**5.4 Hitimisho**

Kwa ujumla, teknolojia ni sehemu muhimu ya maisha ya kisasa na haiwezi kuepukwa. Matumizi yake sahihi yanaweza kukuza elimu, ubunifu, na maadili mema kwa watoto, ilhali matumizi mabaya yanaweza kuathiri vibaya malezi na maendeleo yao.

Ni jukumu la wazazi, walimu, na jamii kwa pamoja kuhakikisha teknolojia inatumika kwa hekima, uwajibikaji, na kwa lengo la kujenga kizazi chenye maadili, nidhamu na maarifa. Kwa kufanya hivyo, teknolojia itabaki kuwa chombo cha maendeleo na si kikwazo cha malezi bora.

official
KITABU Market
www.kitabumarket.co.tz
scan here and enjoy

**KITABU MARKET**

Tovuti mpya ya KITABU MARKET imekuwa hewani karibu juma moja sasa.

Katika tovuti hii, utapata vitabu vya hadithi, maarifa, makala mbalimbali na majarida ya Ngurumo.

Tovuti hii imegawanya maudhui yake katika makundi matatu.

1. KITABU CHA BURE
Katika safu ya Kitabu cha Bure msomaji ataweza kusoma vitabu na majarida na machapisho mengine bure kabisa.

2. MAKTABA
Katika safu ya Maktaba, msomaji atatakiwa kujiunga na uanachama wa Maktaba ndani ya Tovuti hii kwa malipo yatakayopendekezwa. Ndani ya MAKTABA utaweza kusoma vitabu vya aina mbalimbali kadiri ya uwezo wako. Msomaji akilipia ataweza kusoma machapisho hayo katika mfumo wa pdf pasipo kupakua katika simu yake.

3. NUNUA KITABU
Katika safu ya Nunua Kitabu, msomaji ataweza kununua kitabu kwa bei itayoelekezwa katika tovuti. Akishanunua ataweza kukipakua na kukisoma kwa wakati wowote katika simu yake hata akiwa hana bando.

Tembelea sasa tovuti yetu.

https://kitabumarket.co.tz/

Mjuze na mwenzio!

## HAPPY NEW YEAR '11'—Twahir Yusuph

***Ilipoishia***

***"Hata Mimi moyo wangu unaniuma kumtendea haya kijana ambaye sasa amebadilika, sio yule mnyama aliyenifanya niishi hivi leo hii." aliweka tuo, macho pima akiitazama kamera. "Nahuzunika sana kuyaharibu Maisha yake, na kuisambaratisha ndoto ya mwanamke aliyetarajia kuolewa na kijana huyu mwema sasa, pia mwenye upendo sana kwake." akaonesha kutikisa kichwa chake kwa masikitiko.***

***Endelea***

"Ona nilitaka kusahau, kumbe niliwasalimia wazazi wa marehemu wale wawili, na huyu mtarajiwa." alijishika pajini akionesha kama alisahau. "Najua mnanifahamu, japo huenda mkawa hamnikumbuki sababu ya haya mandevu mengi yaliyoubadili uso wangu, au pengine mmeshtushwa na hii sura yangu ya kibishoo baada ya kuiona tena ikiwa inaishi." aliweka tuo akiitazama kamera. "Ndiyo mimi bhana, binadamu mliyeamini kifo kilinichukua siku ile, muungwana mliyeidhurumu haki yake kwa kuwatetea watoto wenu mliowapenda, watoto waliotembea na ukuu wenu hata kwenye usawa wa wao na wengine." Akaweka tuo la pili, sura yake ya upole ikaingiwa simanzi, mboni yake moja ikaanza teririsha chozi alilowahi kulifuta kwa viganja vyake vilivyochafuka kwa damu.

Alipoushusha, ukafikia kinywani, aliiziba midomo yake, alionekana kuyabeba majonzi yaliyomuumiza mno, hisia aliyoionesha ilisaili hilo, licha ya mkono wake mmoja kuendelea kutoliachia shoka lake. *Analia nini sasa huyu baba? Khaa!* "Kama mngeniombaga hata msamaha tu nyakati zile, huenda roho za wan'enu walio makaburini leo hii, ningezitenga na miili yao kistaarabu kabisa, lakini sivyo kama mlivyonilazimisha nyinyi wapuuzi. Kwanini mlishindwa lakini?" Chozi likamtoka tena, nalo akalipangusa. "Masikini ya Mungu mmemponza na yule Daktari wa watu, ila jambo la kupendeza yeye sikumuua kwa fujo. Nilimkatakata kipolepole kabisa, lakini nasikitika zile hela nyingi mlizompa nyakati zile, kesho hatozikwa nazo, na ndizo zimesababisha leo yamkute haya, roho yake inisamehe sana huko nilipoipeleka. Dah!" Akavipatanisha viganja vyake kwa kuweka ishara ya kuomba msamaha, ni kama mtu aliyechanganyikiwa namna alivyoongea, na matendo aliyokuwa akifanya! Ndiyo, alimtaja daktari ambaye Labi Kimati alienda kukutana naye, yule waliyemkuta amefariki muda wanamfuatilia Labi waliyemshuku.

Saa hii muuaji anajisifu kwa kuinyofoa roho yake kistaarabu. Yaani anadhihirisha ni yeye ndiye mhusika wa maiti waliyomkuta nayo, idadi ya aliowaua imeongezeka sasa, dokta ni wa tatu. "Kikubwa nilichokifurahia, ni kifo cha Hakimu yule ambaye kama yasingemuua maradhi aliyougua, huenda na yeye angenipa dhambi ya kumkatakata kama hawa wehu niliomsogezea Mungu kipolepole kwa mikono yangu." akaweka tuo. "Lakini kama Mungu atanipa nafasi ya upendeleo wa kumuomba chochote atachonijibu bila kunisubirisha, basi naomba ampe tena roho arudi kuwa hai, nimfunze haki ya kweli inavyotolewa mshenzi yule, mpuuzi sana yule jamaa, sijui alisomea sheria ili aipindishe!" alionesha kulaumu huku akilichezesha shoka lake. "Ila poleni sana rafiki zangu, maisha yana kasi mno aisee, laiti niliowapenda wasingeendelea kunitokea njozini na maswali yao ya lawama, kuwa kwanini watoto wenu bado wanaishi kwenye Dunia hii iliyowatenga wao na Mimi wanaenipenda bila wenyewe kutaka? Labda hii miaka minne tusiyoonana ingetosha sana kusahau kila kitu. Nisingerudi, ningesubiri zangu nijifie hukohuko. Ila ingekuwaje rahisi kutolikumbuka tukio kama lile, tena vifo vya mtindo ule kwa familia yangu niliyoipenda? Eeh." alilalamika kwa sauti ya upole, huku akijifuta tena machozi.

"Natamani ningekuwa baba mkali kwa binti yangu Mona, mtoto ambaye Mwenyezi alinibariki yeye tu mmoja, baada ya miaka tisa ya ndoa yangu; mimi na mama yake tuliyependana." hapa aliuinua uso wake uliochapika kwa huzuni ambayo sisi hatuijui, na kuitazama tena kamera iliyombele yake. Bado hali ya Labi Kimati ilizidi kuwa tete kitini alipomfunga. "Ila ningefanya nini kwa binti ambaye tayari alishabalekhe! Binti aliyefanya kazi na kujipatia kipato chake mwenyewe, kwamba ningemjengea uzio baina ya moyo wake na mwanaume aliempenda? Mwanaume aliyeshindwa kumficha hata mbele ya mimi baba yake na kunielezea namna upendo

wake unavyomthamini na kutaka awe wake wa maisha! Ningemzuiaje? Mi niliiheshimu furaha ya binti yangu, niliipenda pia." Hapa mboni zake zikaitangaza ghazabu aliyonayo, huku sauti yake ya taratibu ikionesha uchungu.


"Ndiyo huyu Labi Kimati, mkwe wangu, shetani aliyemiliki kabati lenye nguo nyingi nzuri mbele ya moyo wa binti yangu uliooza kwa kumpenda yeye, akijua ni malaika masikini." Aliongea akikishika kidevu cha Labi Kimati na kuutazamisha uso wake uliochakaa mbele ya kamera, ili wamuone vizuri. "Furaha ya binti yangu haikumwamini mwingine zaidi ya huyu, alitabasamu kila kukicha sababu tu mapenzi yalimpa Labi, ningezuia vipi amani ya binti yangu? Baada ya muda mfupi wa mahusiano yao, nilimtaka amlete Labi nyumbani kwangu ili niutambue rasmi uhusiano wao, Mona alinielewa kipenzi changu. Akanipa uhakika tarehe moja ya mwezi unaofuata, Labi na yeye wangenitembelea, zilibaki siku tano tu ili ifike, na mwaka ubadilike. Majira hayakusimama, hatimae yakasalia masaa, ilikuwa usiku wa kuziadhimisha sikukuu za mwaka mpya, tukiwa tumebakisha dakika chache tuingie kwenye kuusheherekea mwaka huo mgeni, huwa ni desturi ya familia yangu kufurahia tukiwa wote pamoja. Mimi, Mona, na Mama yake mrembo. Varandani, televisheni ikiwa wazi, kando yangu akiketi mke wangu kipenzi, sote macho yetu yakikitazama kioo cha Laptop tulichosubiri mwanetu mpendwa, apokee simu yetu ya kuonana tuliyompigia kupitia mtandao wa *WhatsApp*. Sura zetu zilitapakaa tabasamu la furaha mno na shauku ya kumuona." aliibana midomo yake akionesha kama mtu anayetaka kulia kwa sauti.

"Majibu yalirudi, kioo kikaibandika sura nzuri ya Mona, binti yangu mwenye urembo kama wa mama yake akiwa na tabasamu lake zuri tulilolizoea. Mandhari aliyokuwepo yalivutia, palionekana kuwa pa thamani ghari mno, lakini hatukupafahamu ni wapi, baada ya salamu alitueleza kuwa yupo kwa Labi Kimati, amealikwa kwenye tafrija ya kuusheherekea mwaka mpya, itayojumuisha marafiki wengi wa Labi, na yeye akiwemo. Ila hadi muda huo alifika peke yake tu." hapa aliziba midomo yake, akionesha vilevile kama mtu aliyekabwa na kilio cha sauti, ila alijizuia. "Maa..zungumzo yetu yalisheheni furaha nyingi zilizotamani tungeliwepo meza moja saa hiyo, haaa..diiithi zetu ziliunda visa vii..ingi vilivyochipua na vicheko vyetu vya furaha." Kigugumizi kilimshika, huku akionesha tabasamu lenye furaha ya uchungu.

"Tukiwa katikati ya maongezi, Mona alionesha kugeuza shingo yake na kutazama pembeni akiwa mwenye tabasamu, kulekule alipotazama akakielekeza kioo cha simu yake na sisi tuone, alikuwa mkwe wangu akiwasili na wenziwe wawili wakiwa wamependeza sana. Ni Labi, Jax, pamoja na Imraan." hapa sura yake ikaonesha kudhoofika, machozi yakamdondoka. "Wooo..oote watatu walisogea hadi alipo binti yangu Mm...Mona, bila kutarajia marehemu wawili mliowazika, wakaanza kumshikashika kipenzi changu Mo..oona kimahaba." alionekana kushindwa kuongea, kigugumizi kilizidi kumkaba. "Mmm...mona, na hata sisi tukashangazwa, hatukuelewa kinachoendelea, ghafla Labi naye akajumuika nao, akampokonya simu kipenzi changu, huku akiwa anatuonesha paji lake likifurahia vitendo hivyo." akaweka tuo muuaji ambae bado hatujamjua jina, mboni zake zikitiririsha machozi bila kuacha, huku uso wake ukisheheni huzuni.

"Alipiga sana kelele Mona wangu, kwa fujo na mabavu wakaanza kuyachaa..na chana mavazi yake, yote waliyafanya wakiitega kamera ya simu ya binti yetu ituoneshe kila kitu mimi na mama yake, mnajua ilikuwa inauma kiasi gani?" akafoka kwa hasira, uso ukiwa umejaa machozi. "Vijana wale watatu, wakaanza kumuingilia kimmm..mwili Mona wangu, tena wakimrekodi na kutaka wazazi wake tuone." hapa alilipiga piga shoka laje sakafuni kwa uchungu huku akilia.

"Siiii..iiwezi kuuhadithia, au japo kuu..u..elezea tu kwa ufupi, nnn..ni uchungu kiii..aasi gani ambao mioyo yetu mimi na mke wangu uliuhisi.




***Itaendelea...***

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (06)- Na: Eva Mrema

***Ilipoishia...***

**Ilipambwa vizuri na mpambaji stadi. Iliwekwa vinywaji vya kuvutia sana, kiufupi kuelezea kila nilichokiona ni kupunguza utamu wa ule muonekano. Jamaniee! Palipendeza mnoo. Palivutia, palinukia kiasi kwamba nilijikuta mgeni kwenye nyumba ile niliyoijua vizuri.**

***Endelea...***

Alinishika mkono na kuniketisha kitini. Alizunguka na kuketi upande wa pili, upeoni mwa macho yangu. Alipiga mluzi tena kwa mara nyingine. Walikuja wahudumu wawili, mmoja wa kike na mmoja wa kiume, walibeba sahani zenye vyakula, zilizofunikwa na makawa. Waliweka mezani na hapo harufu nzuri ya chakula ilizisabahi pua zangu. Walienda na kurudi kama mwanzo. Walifanya hivyo mara mbili zaidi. Moyoni nilijiuliza maandalizi haya ni ya watu wawili au wangekuja watu wengine kujiunga nasi? Nilikilinda sana kinywa changu na kuropoka. Nilijizuia kama samaki mwenye maji kinywani, ile shauku ya kike ya kuongea kabla ya kutafakari, nilipambana nayo kwa msaada mzuri kutoka kwa 'life coach wangu' ndio nililazimika kumlipa kungwi na kumfanya awe msaada wangu kwenye maisha haswa ya kimahusiano na haiba binafsi. Nimepitia mengi nyuma kabla ya wakati huo, siku nikiwa na hali tulivu ya kihisia nitakusimulieni.



Tuendelee sasa na 'dinner table' ya wachumba. Baada ya maandalizi, walileta sahani mbili tu, zenye kisu, uma na vijiko. Moja iliwekwa kwangu na nyingine kwa Sunche wangu. Waliongezeka wajakazi wengine na kufunua yale makawa kwa wakati mmoja. Machoni kitendo kile kilivutia mno, nimezoea kuona mambo hayo kwenye miziki ya Comoro tu. Baada ya chakula kufunuliwa nilijiambia tu, "Tabita hii ni kufuru" sikufungua kinywa lakini.
"Karibu tule kipenzi" Sunche aliniambia. Nilikaa mkao wa kula, uvumilivu haukunifaa mara hii. "Tunakula peke yetu? Swali langu lilimshangaza sana Sunche. Na nilipobaini jambo hilo nikaongeza neno."Naomba wapishi wako waungane nasi mezani chakula ni kingi sana" "Leo ni mimi na wewe tu kipenzi" Sunche aliongea na kunyanyuka. Alisogea na kiti chake kushoto kwangu. Aliketi na kunitazama machoni, kisha akanituliza. tuliweka chakula tani yetu kwenye sahani moja na kuanza kula bila kufuata sheria zilizowekwa. Kilikuwa kitamu chenye ladha ya kueleweka. Baada ya kula chakula tulikunywa mvinyo kidogo. Alinishika mkono na kuniongoza hadi chumbani kwake. Nje ya mlango aliniomba nifumbe macho yangu. Mie tena! Sikuwa na hiyana wala baya. Nilifumba na kukubali kuongozwa. Akanibeba, hapa wacha nikukumbushe tu, mwili wangu ulikuwa unabebeka jamani. Alinibeba nami nilifumba macho yangu kama nilivyoambiwa.

Nilisikia mlango ukiachama tukaingia, alinishusha chini, aliruhusu nifumbue macho. Jama giza totoro tena. Aliniuliza kama niko tayari kwa mshangao mdogo wa mwisho kwa usiku ule. Nilijibu ndio, yaani nilikuwa kama yule ngamia aliyeingiwa na kisomo kisawasawa. Shingo yangu ilitii kila alichosema Sunche. Nilifumbua macho, chumba kilimeremeta sana. Otea nini? Kuna kitu nikipendacho zaidi. Kipaza sauti kilichosimama kwenye mhimili wake kilizisalimia mboni zangu, ooh! Niliponyoka ubavuni kwa Sunche na kwenda kukishika. Alinitazama huku akitawaliwa na tabasamu. Niliangalia vitu na kuwasha mfumo. Nilijaribu na sauti ilipenya vyema kwenye spika ndogo za muziki zilizofungwa kwenye dari la chumba kile. Mimi siwezi kujizuia kwenye mambo mawili tu, 'kucheza mziki niupendao, na kuimba nionapo kipaza sauti'. Nilikishika kipaza kwa kukibembeleza sana. Nilijiwa na mashairi ya wimbo mpya uliokuwa ukitamba sana. Aliuimba mwanamziki wa kitanzania jina lake, Marlaw'


**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (06) - Na: Eva Mrema

wimbo uliitwa "PENDO LANGU". Kuuimba ubeti wa kwanza kulimfanya Sunche anikaribie. Alinishika na kwa ushirikiano tulicheza kimahaba. Mkimuona yule aliyesema usiku mrefu, mwambieni angeniongezea muda na kunipunguzia uchovu nyakati tamu. Nilichoka sana. Baada ya mambo yote. Tulijipa muda wa ukimya na kuiacha mioyo yetu izungumze. Tuliishia kutazamana tu, hakuna aliyekuwa na papara na mwenzake tulijituliza na mwishowe usingizi ukatuchukua mateka.

Alfajiri nilikurupuka na kuondoka. Ukizingatia sana unaweza kusema nilitoroka. Bahati nzuri nyumbani kwa Sunche sio kijijini, nilipata pikipiki kirahisi sana.
Nilipita nyumbani kwangu nikachukua kila nilichokihitaji kisha nikaondoka. Kama kawaida asubuhi hua siendeshi gari nakimbia kama mwizi hadi ofisini kwangu. Na siku hii kama siku nyingine tu, nilikimbia na kufika mapema ofisini; niliweka sawa mambo yangu na kuketi kwenye kiti changu cha kuzunguka. Muda wa kazi uliwadia, akili yangu ilikuwa tayari kwa kazi. Mshale wa dakika ulikwenda taratibu sana kwenye saa iliyopo ukutani mwa ofisi yangu. Nilijaribu kuangalia kwenye saa ya mkononi mambo ni yaleyale. Saa nne asubuhi simu yangu iliita. Niliikata na kutuma ujumbe, siruhusiwi kuongea na simu ndani ya ofisi.

Alikuwa Sunche aliyepiga simu, aliupokea ujumbe wangu ila hakuujibu. Niliitazama simu kila sekunde kama vile nilikuwa nakaanga yai kwenye moto wa kuni. Nilitekeleza majukumu yangu, muda wa chakula cha mchana nilielekea mgahawani niliketi mahali nilipopazoea. Tofauti na siku nyingine siku hii nilihudumiwa bila kusikilizwa. Mezani yalitangulia maua, sio ya kichina ni maua halisi ya waridi. Yalinukia vizuri kiasi nilitamani kuyakwanyua niyalambe. Nilijituliza tuli, kililetwa chakula mezani. Ni chakula nipendacho ila mpango wangu wa siku hiyo haukumudu gharama ya chakula kile. Nilimwambia muhudumu aangalie vizuri labda kachanganya maelezo. Aliangalia na kunijibu kuwa hajachanganya alikuwa sahihi. Nilitaka kumuuliza swali lingine ila akawa tayari kaondoka. Nilikumbuka Sunche alinipigia simu muda uliopita. Nilishika simu na kumpigia kabla hata sijala chakula. Mlio wa simu niujuao vizuri ulisikika nyuma ya mgongo wangu. Kabla sijageuka nilikumbatiwa shingoni kutokea nyuma, bado nilikuwa nimekaa kwenye kiti changu. Alinibusu shavuni na kuniuliza hali yangu. Tulisabahiana baada ya mipasho kidogo; chekacheka za hapa na pale tulipata chakula cha mchana pamoja. Nusura nikawie kazini kisa mahaba ya Sunche. Wakati tunaagana nilimpatia funguo na kumuomba aipitie gari yangu tulipoiacha jana.
Ule mgahawa tulipokula, ulitumiwa karibu na wafanyakazi wote wa pale ofisini. Basi bwana, kila lililojiri mgahawani nikalikuta tayari limenitangulia kufika ofisini. Nilijali basi? Nikaendelea na mambo yangu. Siku zilisonga tukiwa katika huba zito na nono mimi na Sunche wangu. Kazini niliitwa 'muke ya muzungu'. Nilikuwa katika ushwari wa hali ya kihisia. Harara, chunusi na ufubavu vilitoweka kwenye ngozi yangu.
Niliwakawaka balaa. Tulijipa muda kabla tukutane kimwili. Ndio tulikubaliana maana kila mmoja wetu alishaumia huko kabla. Tulitaka tu kuhakikisha kama tuko sahihi katika maamuzi tuliyochukua. Miezi mitatu ni mingi kwa watu wazima kupimana ustahimilivu.

Tuliridhiana. Sio moyoni tu, mwilini pia tulishibana. Asili yangu Mngoni, bila shaka unaelewa vile tunafanyaga kwenye upande wa *malavidavi*, nimechezwa mkoleni na *mizungu* yote ya asili nilifunzwa. Si mvivu wa kujifunza, *mizungu* ya kigeni pia niliimudu. Sikumdhalilisha kungwi wangu, dozi ya kwanza nusura imuue mgonjwa. Nilimkaribisha Sunche Tanzania. Likizo ya siku mbili za kujuana kiundani, haikuisha kinyonge. Sunche aliniomba jambo kubwa sana. Binafsi liliniogofya, si mara ya kwanza kupitia hali hii, ilinikumba miaka miwili iliyopita na kuniweka katika hali ngumu sana ya kihisia. Nilikonda, niliugua na kujipoteza kabisa. Maumivu niliyopitia wakati ule, simuombei hata adui yangu ayapitie.

Na mimi nilikula KIAPO… "Kama itatokea mara nyingine, kujikuta katikati ya mapenzi na ndoa, basi nitachagua mapenzi na kuipuuza kabisa ndoa". Sunche alitaka kunioa haraka sana. Kwa ulimi laini akaniomba anioe. Sikuwa na jibu, machozi yalianza kunibubujika nilitoka karibu yake na kukimbilia msalani. Nilifungulia maji na kuanza kulia kwa kwikwi.

***Itaendelea...***

**BURUDIKA**
www.kitabumarket.co.tz

# Tangazo




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com